UCHUMI WETU

TOLEO NA. 06, OKTOBA 2026



NENO LA GAVANA



Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Kama ilivyo ada, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inawaletea Jarida la UCHUMI WETU la kila robo mwaka, ili kuwapa taarifa na elimu ya masuala ya uchumi yanayotekelezwa na taasisi za fedha ndani na nje ya nchi yetu. Ninayo furaha ya kukukaribisha katika toleo hili la sita.

Kabla ya kugusia masuala ya uchumi na fedha, napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali anayoiongoza, kwa kuendelea kutoa miongozo mbalimbali yenye lengo la kuimarisha uchumi wa nchi yetu, na kuanza vizuri utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050. Aidha, nampongeza kwa dhati Mhe. Deogratius John Ndejembi kwa kuteuliwa na kuthibitishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vile vile, natumia nafasi hii kuishukuru Jumuiya ya Huduma Jumuishi za Fedha (AFI) kwa kuipatia Benki Kuu ya Tanzania Tuzo ya Azimio la Maya (Maya Declaration Award), kutokana na utekelezaji mzuri wa azimio la kuendeleza huduma jumuishi za fedha nchini. Tuzo hiyo ilitolewa Septemba 2026 wakati wa Mkutano wa Dunia wa Sera wa AFI wa mwaka 2026 (AFI Global Policy Forum – GPF 2026), uliofanyika Port Moresby, Papua New Guinea.

Kuhusu hali ya uchumi nchini, takwimu zinaonesha kwamba uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar uliendelea kuimarika na kukua kwa kasi iliyopangwa kwa mwaka 2026. Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 6.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, na unakadiriwa kukua kwa zaidi ya asilimia 6 katika robo ya pili na ya tatu, ukichangiwa zaidi na kuimarika kwa huduma za kifedha, uzalishaji viwandani, uwekezaji katika miundombinu na huduma za jamii. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 6.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, huku ukuaji ukikadiriwa kuzidi asilimia 7 katika robo ya pili na ya tatu. Ukuaji huo umechangiwa zaidi na shughuli za utalii, ujenzi na miradi ya umwagiliaji. Uchumi wetu unatarajiwa kuendelea kukua licha ya uwepo wa vihatarishi vinavyotokana na ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, kuvurugika kwa minyororo ya ugavi na athari za mvua za El Niño.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa juu kidogo kutokana na migogoro inayoendelea Mashariki ya Kati. Kwa Tanzania Bara, mfumuko wa bei umeendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, licha ya kuongezeka hadi asilimia 4.3 mwezi Septemba 2026, kutoka wastani wa asilimia 4.1 kwa robo mwaka inayoishia Juni 2026. Hata hivyo, mfumuko wa bei umeendelea kuwa ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa asilimia 8 kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na asilimia 3 hadi 7 kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 5.6 mwezi Septemba 2026 kutoka asilimia 6 mwezi Julai 2026. Hata hivyo, kiwango hicho kilikuwa juu ya wastani wa asilimia 5.5 katika robo mwaka iliyoishia Juni 2026, na lengo la muda wa kati la asilimia 5.

Hali ya ukwasi imeendelea kuakisi mahitaji ya shughuli za kiuchumi hadi Septemba 2026. Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuongezeka kwa kasi, kufikia wastani wa asilimia 32.5 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2026. Sekta ya kibenki iliendelea kuwa imara, ikichangiwa na uwepo wa mitaji, ukwasi wa kutosha, pamoja na faida. Mikopo chechefu ilishuka hadi asilimia 2.5 mwezi Agosti 2026, kiwango ambacho ni ndani ya ukomo unaohimilika kimataifa wa asilimia 5. Wakati huohuo, mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi na uthabiti wa hali ya juu, huku idadi na thamani ya miamala ikiongezeka.

Sekta ya nje imeendelea kuwa tulivu licha ya kuongezeka kwa changamoto za migogoro ya kisiasa duniani. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka kidogo kutokana na athari za misukosuko ya kiuchumi ya nje, na kufikia asilimia 2.5 ya Pato la Taifa katika mwaka ulioishia Septemba 2026, ikilinganishwa na asilimia 2.4 ya Pato la Taifa katika mwaka ulioishia Juni 2026. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha, ikiwa zaidi ya dola za Marekani bilioni 6.0, yenye uwezo wa kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa miezi 4.3.

Napenda kuwajulisha kwamba toleo hili la Jarida letu limesheheni habari na taarifa nyingi kuhusu uchumi wetu, uchumi wa kimataifa na huduma za fedha. Vile vile, toleo hili linatoa elimu kuhusu utunzaji wa fedha na athari zinazotokana na uharibifu wa fedha zetu. Katika hili, Kifungu cha 332A cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Toleo la Marejeo la mwaka 2023, kinaeleza wazi kuwa mtu ambaye anaharibu, anachana, anakata au kwa namna nyingine anachanachana noti au fedha halali kwa makusudi bila mamlaka hayo, anatenda kosa. Hivyo, nawasihi wananchi wajenge tabia ya kutunza vyema fedha zao kwani ni tunu ya Taifa yetu.

Kwa kuhitimisha, napenda kukukaribisha tena msomaji wetu katika toleo hili la sita la Jarida la UCHUMI WETU. Nina imani kuwa kupitia makala na habari mbalimbali zilizomo kwenye jarida hili, utapata maarifa na uelewa utakaosaidia katika kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Nawatakia wote usomaji mwema.

Emmanuel Mpawe Tutuba
Gavana, Benki Kuu ya Tanzania.

MEZA YA MHARIRI MKUU



Victoria Msina

Meneja, Mawasiliano
Benki Kuu ya Tanzania.

Ndugu Msomaji Wetu,

Karibu katika Jarida la Uchumi Wetu, Toleo la Sita. Ni furaha kubwa kukuletea tena jarida hili linalolenga kukuelimisha na kukupatia taarifa mbalimbali kuhusu masuala ya uchumi na sekta ya fedha nchini, hususan yale yanayoratibiwa na kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa mujibu wa sheria.

Katika toleo hili tumekuandalia makala na taarifa mbalimbali zenye umuhimu Taifa na wananchi kwa ujumla, miongoni mwao ikiwa ni umuhimu wa utunzaji wa noti, matakwa ya kisheria kuhusu utunzaji wa noti, pamoja na namna Benki Kuu inavyomuunga mkono Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050.

Aidha, kupitia ushirikiano wetu na wadau mbalimbali wa sekta ya fedha, jarida hili linakupa fursa ya kupata habari na taarifa kutoka taasisi muhimu zinazochangia maendeleo ya sekta hiyo. Miongoni mwa taasisi hizo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Bodi ya Bima ya Amana (DIB) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

Katika kuendelea kujenga na kuimarisha uhusiano na jamii inayotuzunguka, Benki Kuu huandaa mikakati thabiti na kutumia fursa mbalimbali kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake, huku ikipokea maoni, ushauri na mapendekezo kutoka kwa wadau wake kwa lengo la kuboresha zaidi huduma zinazotolewa. Katika toleo hili, utaona pia namna wanawake wa Benki Kuu ya Tanzania walivyogusa maisha ya jamii kwa kushiriki katika ujenzi wa uwanja wa michezo katika Shule ya Msingi Bunge, jijini Dar es Salaam.

Ni matumaini yangu kuwa, kupitia jarida hili, utapata fursa ya kuifahamu na kuielewa zaidi sekta ya uchumi na fedha, kupitia makala zilizoandaliwa ikiwemo vibonzo, habari-picha na mashairi ndani ya Jarida la Uchumi Wetu, Toleo la Sita.

Tunathamini maoni na ushirikiano wako. Endapo una maoni, ushauri au mapendekezo kuhusu jarida hili, tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: ***botcommunications@bot.go.tz***

Nakutakia usomaji mwema.

RIBA YA BENKI KUU KUBAKIA ASILIMIA 6.25

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeamua Kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kubaki asilimia 6.25 kwa robo ya nne ya mwaka 2026, hatua inayolenga kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi katika Tanzania Bara na Zanzibar.

Uamuzi huo ulitangazwa, Oktoba 8, 2026, na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, baada ya Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) kukutana Oktoba 7, 2026.

Gavana Tutuba alisema uchumi wa Tanzania Bara uliendelea kuimarika, ukikua kwa asilimia 6.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, huku ukitarajiwa kuzidi asilimia 6 katika robo ya pili na ya tatu. Zanzibar nayo ilikua kwa asilimia 6.7 katika robo ya kwanza, huku ukuaji ukitarajiwa kuzidi asilimia 7 katika robo ya pili na ya tatu.

Kwa upande wa mfumuko wa bei, Tanzania Bara uliendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, licha ya kuongezeka hadi asilimia 4.3 mwezi Agosti 2026, kutoka wastani wa asilimia 4.1 katika robo iliyoishia Juni. Zanzibar, kwa upande mwingine, mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 5.6 mwezi Agosti, kutoka asilimia 6 mwezi Julai, ingawa uliendelea kuwa juu ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.

Gavana alisema ukuaji wa uchumi katika maeneo yote mawili umechangiwa na shughuli mbalimbali. Tanzania Bara imeendelea kunufaika na huduma za kifedha, uzalishaji viwandani, uwekezaji katika miundombinu na huduma za jamii, wakati Zanzibar imeendelea kuchangiwa zaidi na utalii, ujenzi na miradi ya umwagiliaji.

Sekta ya fedha iliendelea kuwa imara, huku mikopo kwa sekta binafsi ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 32.5 katika robo iliyoishia Septemba 2026. Mikopo chechefu ilibaki katika kiwango cha asilimia 2.5 mwezi Agosti, chini ya ukomo wa asilimia 5.

Katika sekta ya nje, Tanzania iliendelea kuwa na akiba ya fedha za kigeni ya zaidi ya dola bilioni 6, inayotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.3. Tanzania Bara ilikabili nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ya asilimia 2.5 ya Pato la Taifa katika mwaka ulioishia Septemba, huku Zanzibar ikiendelea kuwa na ziada ya urari wa malipo ya kawaida, ikisaidiwa zaidi na mapato ya utalii.

Hata hivyo, Gavana alisema uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar unaendelea kukabili vihatarishi vinavyotokana na mgogoro wa Mashariki ya Kati, kupanda kwa bei za mafuta na mbolea duniani, kuvurugika kwa minyororo ya ugavi pamoja na athari zinazoweza kutokana na mvua za El Niño.

Aliongeza kuwa BoT itaendelea kufuatilia mwenendo wa uchumi na kuchukua hatua stahiki za kisera kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki katika viwango vinavyolengwa huku ukuaji wa uchumi ukiendelea.

Mkutano ujao wa MPC utafanyika Januari 6, 2027, na uamuzi kuhusu CBR kwa robo ya kwanza ya mwaka 2027 utatangazwa siku inayofuata.



Gavana Emmanuel Tutuba akifafanua jambo kuhusu Riba ya Benki Kuu katika kikao na waandishi wa habari pamoja viongozi wa mabenki kilichofanyika tarehe 8 Oktoba 2026 BoT jijini Dar es Salaam.



Waandishi wa habari na viongozi wa mabenki katika kikao na Gavana Emmanuel Tutuba kilichofanyika BoT jijini Dar es Salaam tarehe 8 Oktoba 2026.




Kutoka kulia ni Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi, Dkt. Suleiman Missango, Naibu Gavana, Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, Gavana Emmanuel Tutuba, Kaimu Mwenyekiti wa Umoja wa Mabenki ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Equity, Bi. Isabela Maganga, na Mkurugenzi wa Umoja wa Mabenki Tanzania, Bi. Tuse Joune.

MUHTASARI WA TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA KWA ROBO YA NNE YA MWAKA 2026

08 OKTOBA 2026

RIBA YA BENKI KUU KWA ROBO YA NNE YA 2026 YABAKIA **6.25%**



UKUAJI WA UCHUMI
Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa 6.0%, huku Zanzibar ukikua kwa 6.7% katika robo ya kwanza ya 2026, na ukuaji ukitarajiwa kuongezeka zaidi katika robo ya pili na ya tatu.

URARI WA MALIPO YA KAWAIDA
Tanzania Bara:
Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka kidogo hadi 2.5% ya Pato la Taifa katika mwaka ulioishia Septemba 2026
Zanzibar:
imeendelea kuwa na ziada ikichangiwa zaidi na mapato ya utalii.

SEKTA YA KIBENKI
Mikopo chechefu ilifikia 2.5% mwezi Agosti 2026, kiwango ambacho ni chini ya ukomo unaohimilika wa 5%.

MIKOPO KWA SEKTA BINAFSI
Imeendelea kuongezeka kwa kasi, kufikia wastani wa 32.5% katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2026.

AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI
imezidi dola bilioni 6, kiasi kinachotosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa miezi 4.3.

MFUMUKO WA BEI
Tanzania Bara:
Umebaki ndani ya lengo la kitaifa la 3%-5%, licha ya kuongezeka hadi 4.3% mwezi Agosti 2026 kutoka 4.1% robo ya pili ya 2026.
Zanzibar:
Umepungua hadi 5.6% mwezi Agosti 2026 kutoka asilimia 6.0 mwezi Julai 2026

KIELELEZO CHA FAIDA REJEA KUIMARISHA UWAZI NA UFANISI WA SOKO LA DHAMANA ZA SERIKALI



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Kielelezo cha Faida Rejea ya Dhamana za Serikali uliofanyika tarehe 07 Agosti 2026 katika ofisi za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Dar es Salaam.



Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), CPA. Nicodemas Mkama,akiziungumza katika hafla ya uzinduzi wa Kielelezo cha Faida Rejea ya Dhamana za Serikali uliofanyika tarehe 07 Agosti 2026 katika ofisi za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Dar es Salaam.



Naibu Gavana wa Sera za Uchumi na Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Kielelezo cha Faida Rejea ya Dhamana za Serikali uliofanyika tarehe 07 Agosti 2026 katika ofisi za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Dar es Salaam.

Wakati Serikali ikifungua milango kwa wawekezaji kutoka mataifa yote duniani kushiriki katika hatifungani, Benki Kuu imezindua kielelezo cha faida rejea ambacho kinarahisisha mwekezaji kulifahamu soko.

Hafla ya uzinduzi huo iliongozwa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, ambaye alisema Kielelezo cha Faida Rejea ya Dhamana za Serikali (Tanzania Sovereign Yield Curve) kitaongeza uwazi, ushindani na ufanisi katika soko la Dhamana za Serikali.

Gavana Tutuba aliyasema hayo katika hafla ya uzinduzi wa Kielelezo hicho uliyofanyika katika ofisi za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Dar es Salaam Agosti 7, 2026.

Gavana alisema Kielelezo hicho kinachotokana na miamala halisi katika soko la upili kitawawezesha wawekezaji kufuatilia mwenendo wa faida na kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

“Kielelezo hicho pia kitakuwa rejea muhimu katika kupanga bei za mikopo, mikopo ya nyumba na hatifungani za kampuni, kwa kutumia viwango rejea visivyo na hatari (risk-free benchmark rates),”alisema Gavana Tutuba.

Gavana Tutuba aliongeza kuwa kitasaidia kuvutia mitaji ya kigeni na kuongeza ushindani katika soko la dhamana za serikali, huku akisisitiza kuwa soko hilo lina mchango muhimu katika kuiwezesha Serikali kupata fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo.

“Ushiriki wa wadau katika soko la Dhamana za Serikali ni muhimu katika kuiwezesha Serikali kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na hivyo kuchangia katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050,” alisema.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, akizindua Kielelezo cha Faida Rejea ya Dhamana za Serikali tarehe 07 Agosti 2026 katika ofisi za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Dar es Salaam.

Vilevile, alisisitiza kuwa Kielelezo hicho ni kioo kinachoakisi matarajio ya soko kuhusu mwelekeo wa ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei na sera ya fedha, huku kwa upande wa Benki Kuu kikitarajiwa kuimarisha utekelezaji wa sera ya fedha inayotegemea viwango vya riba (interest rate-based monetary policy transmission).

Kwa upande wake Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Madeni wa Wizara ya Fedha, Bw. Japhet Justine, alieleza kuwa Kielelezo hicho ni hatua muhimu na ya kihistoria katika kuendeleza soko la Dhamana za Serikali na kujenga miundombinu ya masoko inayokidhi viwango vya kimataifa.

Kamishna huyo alisisitiza kuwa Kilelezo hiki ni suluhisho la changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa taarifa za kutosha kuhusu viwango halisi vya faida vinavyotokana na mauzo na manunuzi ya Dhamana katika soko la upili, hali iliyokuwa ikifanya iwe vigumu kupanga bei sahihi za dhamana.

Awali, Naibu Gavana wa Sera za Uchumi na Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania, Dkt. Yamungu Kayandabila, alitambua na kupongeza mchango wa wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania, pamoja na utaalamu uliotolewa na Ofisi ya Hazina ya Marekani (U.S. Treasury Department), katika kufanikisha uundwaji wa Kielelezo hicho, akisisitiza umuhimu wa kuendelea kuimarisha ushirikiano huo wa kitaalamu katika juhudi za kuendeleza na kuimarisha soko la Dhamana za Serikali nchini.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa naAfisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), CPA. Nicodemas Mkama, Mkurugenzi Mtendaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Bw. Peter Nalitolela, viongozi na watumishi wa Wizara ya Fedha, Wawakilishi wa Idara ya Hazina ya Marekani na wadau wengine wa sekta ya fedha nchini.

SERIKALI YAAGIZA ELIMU YA FEDHA ICHOPEKWE KIKAMILIFU KATIKA MITAALA YA ELIMU YA JUU



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wanu Hafidh Ameir (Katikati), baada ya kuzindua Mwongozo wa Kuchopeka Elimu ya Fedha katika mitaala ya elimu ya juu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi iliyofanyika Oktoba 02, 2026 jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Naibu Gavana wa BoT, Bi. Sauda Msemo na Kulia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi.

Serikali imezielekeza taasisi za elimu ya juu, vyuo vya ufundi na vile vya mafunzo ya ufundi stadi kuhakikisha elimu ya fedha inachopekwa kikamilifu katika mitaala yao ili kuwawezesha wahitimu kuwa na ujuzi wa kusimamia fedha, kufanya maamuzi sahihi ya kifedha na kujilinda dhidi ya vitendo vya ulaghai.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Bi. Wanu Hafidh Ameir, alisema taasisi hizo zinapaswa kuhakikisha elimu ya fedha inakuwa sehemu ya ufundishaji, tathmini na mifumo ya uhakiki wa ubora wa elimu, huku kukiwa na matokeo yanayopimika katika mabadiliko ya mwenendo wa kifedha wa wanafunzi.

Ametoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa Mwongozo wa Kuchopeka Elimu Ya Fedha katika Mitaala ya Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini uliofanyika Oktoba 02 2026 katika ofisi BoT jijini Dar es Salaam.

“Mwongozo huu unapaswa kuakisiwa katika mitaala, mbinu za ufundishaji na tathmini ili kuwawezesha wanafunzi kutumia maarifa ya kifedha katika maisha yao ya kila siku na kufanya maamuzi yenye uwajibikaji wanapoingia katika soko la ajira,” alisema.

Amezitaka taasisi hizo kutenga rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa mwongozo huo kupitia mipango na bajeti zao za mwaka, badala ya kutegemea pekee ufadhili kutoka nje.

Aidha, amezitaka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kufuatilia mara kwa mara utekelezaji wa mwongozo huo ili kubaini mapungufu na kupendekeza maboresho.

Aliongeza kuwa elimu ya fedha ni muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kujenga uchumi wenye ushindani na uzalishaji mkubwa unaoungwa mkono na nguvu kazi yenye ujuzi.

Alisema licha ya huduma za kifedha za kidijitali kurahisisha shughuli za kifedha, ukosefu wa uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya fedha unaweza kuwaweka vijana na familia zao katika hatari ya kufanya maamuzi yenye gharama kubwa.

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, amesema mafanikio ya mwongozo huo mpya hayatategemei uwepo wake pekee, bali utekelezaji wake kwa ufanisi na athari utakazokuwa nazo katika kuboresha mwenendo wa kifedha wa wahitimu.

Alisema elimu ya fedha ni muhimu katika kujenga mfumo wa fedha ulio imara, salama na shirikishi, akibainisha kuwa upatikanaji wa bidhaa za kifedha na huduma za kidijitali pekee hautoshi bila kuwa na maarifa ya kuelewa gharama, manufaa na hatari zinazohusiana na huduma hizo.



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wanu Hafidh Ameir, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Mwongozo wa Kuchopeka Elimu ya Fedha katika mitaala ya elimu ya juu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi iliyofanyika Oktoba 02, 2026 jijini Dar es Salaam.



Naibu Gavana wa BoT , Bi. Sauda Msemo akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Mwongozo wa Kuchopeka Elimu ya Fedha katika mitaala ya elimu ya juu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi iliyofanyika Oktoba 02, 2026 jijini Dar es Salaam.

“Mwongozo huu mpya utapanua elimu ya fedha hadi katika taasisi za elimu ya juu, vyuo vya ufundi na vile vya mafunzo ya ufundi stadi, hivyo kukamilisha kiungo muhimu katika mpango wa kitaifa wa elimu ya fedha,” alisema.

Alisema Serikali, kupitia Mfumo wa Tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa mwaka 2023—2028(National Financial Inclusion Framework), imeipa kipaumbele elimu ya fedha na ulinzi wa mlaji wa huduma za fedha kama nguzo muhimu za ujumuishi endelevu wa huduma za fedha.

Alibainisha kuwa hadi kufikia mwishoni mwa Juni mwaka huu, jumla ya waelimishaji wa fedha 1,736 walikuwa wamepatiwa mafunzo na kuthibitishwa, huku watu 1,882,443 wakiwa wamefikiwa na elimu ya fedha kupitia njia mbalimbali.

Aliongeza kuwa Serikali, kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, imejumuisha elimu ya fedha katika mitaala iliyoboreshwa ya elimu ya msingi na sekondari. Aidha, mwezi Mei 2026, BoT na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) zilisaini makubaliano ya kutoa elimu ya fedha kwa wanafunzi wa elimu ya juu kupitia mfumo wa kidijitali wa SIPA unaounganishwa na akaunti zao.

Kwa upande wake, Kamishna wa Idara ya Fedha za Nje katika Wizara ya Fedha na Mipango ya Zanzibar, Bw. Yussuf Ibrahim Yussuf, alisema ujumuishaji wa elimu ya fedha katika mitaala ya elimu utawawezesha vijana kuwa na ujuzi wa kufanya maamuzi sahihi ya kifedha na kutumia fursa za kiuchumi kwa ufanisi. Alisema mpango huo unaunga mkono malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021/22–2025/26, ambayo yanatoa kipaumbele kwa maendeleo ya rasilimali watu, ujumuishi wa huduma za fedha na uchumi wa buluu.

Naye Mkurugenzi wa Ustawi na Huduma Jumuishi za Kifedha BoT, Bw. Kennedy Komba, alisema mwongozo huo utaweka mfumo wa pamoja wa kufundisha na kutathmini elimu ya fedha, hivyo kuondoa mifumo iliyotawanyika na kuweka mfumo wa kujifunza wenye mpangilio na unaoeleweka.

Alisema mwongozo huo utawasaidia wanafunzi kuelewa masuala ya mikopo, kusimamia madeni, kulinda taarifa zao binafsi na kufanya maamuzi sahihi kuhusu uwekezaji.



UJUMUISHAJI: BoT YAZINDUA MACHAPISHO MAALUMU KWA WASIOONA

Katika kuhakikisha ujumuishaji katika elimu ya fedha unaongezeka na kuyafikia makundi yote, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imezindua rasmi machapisho ya nukta nundu kwa ajili ya wasioona (Braille).

Uzinduzi huo ni miongoni mwa mikakati ya BoT katika kutekeleza DIRA YA TAIFA 2050 ambapo uchumi wa nchi unatakiwa kufika thamani ya Dola za Kimarekani trilioni moja.

Akizungumza Agosti 20, 2026, wakati wa uzinduzi wa machapisho hayo, Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, amesema hatua hiyo inaonesha dhamira ya taasisi hiyo kuhakikisha taarifa kuhusu uchumi, huduma za kifedha na majukumu ya Benki Kuu zinapatikana katika mifumo inayozingatia mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii.

Alisisitiza kuwa ujumuishi wa kifedha haupaswi kuishia kwenye kufungua akaunti za benki au kupata huduma za kifedha pekee, bali unapaswa pia kuhakikisha kila mwananchi anapata taarifa anazohitaji ili kufanya maamuzi sahihi ya kifedha.

“Upatikanaji wa taarifa unazidi kuwa muhimu katika dunia ambayo uelewa wa masuala ya kifedha una mchango mkubwa katika maamuzi kuhusu kuweka akiba, kuwekeza, kukopa, kutumia huduma za kifedha na kujilinda dhidi ya udanganyifu wa kifedha”., alieleza

Aidha, Dkt. Mahfoudh alitoa wito kwa taasisi za umma, sekta binafsi, taasisi za elimu na wadau wengine kutathmini namna wanavyotoa taarifa na kujihoji iwapo huduma na njia zao za mawasiliano zinazingatia mahitaji ya watu wenye aina mbalimbali za ulemavu

“Taasisi zinapaswa kujiuliza kama taarifa wanazotoa zinawafikia watu wote, kama mtu mwenye ulemavu wa kuona anaweza kuzipata kwa urahisi, na kama huduma zao zimezingatia mahitaji ya watu wenye aina mbalimbali za ulemavu,” alisema Dkt. Mahfoudh.

Machapisho hayo yanahusu mada mbalimbali, zikiwemo uanzishwaji wa benki na taasisi za fedha, usimamizi wa fedha binafsi, uwekezaji, taarifa za mikopo, amana, mifumo ya malipo, utoaji wa leseni za biashara na miongozo kwa watoa huduma ndogo za kifedha, pamoja na historia na majukumu ya Benki Kuu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wasioona Zanzibar (ZANAB), Bi. Fatma Dijaa, aliishukuru Benki Kuu kwa kuendelea kuwafikia wasiiona hapa nchini na kupitia machapisho haya ya Braille watanufaika kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kifedha.

Katibu wa Jumuiya ya Wasioona Tanzania (TBA), Bw. Iddi Damka, aliipongeza BoT kwa kutengeneza machapisho hayo ambayo yatapanua wigo wa elimu kwa umma.

Uzinduzi huo a ulihudhuriwa pia na Wafanyakazi na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kishirikishi cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) pamoja na viongozi na wafanyakazi wa BoT.





Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, akikabidhi chapisho la Braille lenye historia ya Benki Kuu kwa Katibu wa Jumuiya ya Wasioona Tanzania (TBA), Bw.Iddi Damka, mara baada ya uzinduzi wa machapisho hayo.



Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, akikabidhi chapisho la Braille lenye historia ya Benki Kuu kwa Katibu wa Jumuiya ya Wasioona Tanzania (TBA), Bw.Iddi Damka, mara baada ya uzinduzi wa machapisho hayo.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wasioona Zanzibar, Bi. Fatma Dijaa, akitoa neno la shukrani mara baada ya uzinduzi wa Machapisho ya Braille kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kuona uliofanyika Agosti 20 2026 katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam.

NAMNA BENKI KUU INAVYOTEKELEZA DIRA YA TAIFA YA MWAKA 2050



Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha sekta ya fedha na uchumi mkuu vinakuwa nguzo muhimu katika kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050, ikilenga kujenga uchumi wa kipato cha kati cha juu, mseto, himilivu, jumuishi na unaoshindana katika soko la ndani na la kimataifa.

Katika dira hiyo inayolenga kuleta maendeleo ya nchi ya muda mrefu BoT ina jukumu muhimu katika kuhakikisha mazingira ya uchumi na sekta ya fedha yanakuwa imara na wezeshi kwa uwekezaji, uzalishaji na biashara.
Akizungumza kuhusu nafasi ya Benki Kuu katika utekelezaji wa Dira hiyo, Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba amesema jukumu la taasisi hiyo ni kuhakikisha sera ya fedha na usimamizi wa sekta ya fedha vinaendana na malengo mapana ya maendeleo ya Taifa.

"Kwa Benki Kuu, Dira ya 2050 ina maana ya kuchangia utekelezaji wa malengo yake kwa kuoanisha na kufunganisha malengo na vipaumbele vya mpango mkakati wa Benki Kuu na vipaumbele vya maendeleo ya Taifa," anasema Gavana Tutuba.

Kwa mujibu wa mpango huo, Benki Kuu inatarajiwa kuendelea kuandaa na kutekeleza sera ya fedha, kusimamia taasisi za fedha, kulinda utulivu wa kifedha na uchumi pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa mazingira yanayowezesha ukuaji endelevu wa uchumi.

Utulivu wa bei

Moja ya maeneo makubwa ambayo Benki Kuu imeyapa kipaumbele ni kudumisha utulivu wa bei. Hii inahusisha kutumia sera ya fedha kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki katika viwango vinavyodhibitika (digiti moja), jambo ambalo ni muhimu kwa wananchi, wafanyabiashara na wawekezaji kufanya maamuzi ya kiuchumi kwa uhakika zaidi.

Gavana Tutuba anaeleza kuwa Benki Kuu inalenga kutumia tafiti, takwimu na ubunifu katika kuimarisha ufanisi wa sera ya fedha.

"Hatua hii itapelekea utulivu wa mfumko wa bei katika kiwango cha chini baina ya asilimia 3 hadi 5, ukuaji wa uchumi jumuishi kwa wastani wa asilimia 7.2, utulivu wa kiwango cha riba ya siku saba katika soko la fedha na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi," anasema.

Miongoni mwa malengo ya BoT katika uchumi ni kuwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2026/27, lengo la mfumuko wa bei ni kubaki kati ya asilimia 3 na 5 kila mwaka, huku ukuaji halisi wa Pato la Taifa kuongezeka kutoka asilimia 7.2 hadi asilimia 10.5 ifikapo 2030/31.

Kuimarisha fedha za kigeni

Eneo lingine ni kuimarisha akiba ya fedha za kigeni ili kuhakikisha nchi ina uwezo wa kukidhi mahitaji yake ya malipo ya nje na kuongeza uhimilivu wa uchumi.

Kwa mujibu wa Gavana, Benki Kuu itaendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza vyanzo vya fedha za kigeni, ikiwamo kusaidia ongezeko la uzalishaji wa dhahabu nchini na kuongeza akiba ya taifa ya dhahabu.

"Hatua hii itaongeza kiwango cha kutosha cha akiba ya fedha za kigeni kufikia zaidi ya miezi minne ya kugharamia uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi," anasema Gavana Tutuba.

Gavana Tutuba anaeleza kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Benki Kuu imeweka shabaha ya akiba ya fedha za kigeni kuwa sawa na angalau miezi minne ya uagizaji bidhaa kutoka nje.

Sekta binafsi kupata fedha zaidi

Dira 2050 inahitaji uchumi unaoongozwa zaidi na sekta binafsi, jambo linaloifanya sekta ya fedha kuwa kiungo muhimu katika upatikanaji wa mitaji na mikopo.

Benki Kuu imepanga kuimarisha utulivu wa sekta ya fedha na uchumi mkuu ili kujenga mazingira mazuri kwa wafanyabiashara, wawekezaji na wazalishaji kupata fedha.

"Benki Kuu itarahisisha upatikanaji wa fedha na mitaji kwa wafanyabiashara, wawekezaji na wazalishaji kwa kuimarisha utulivu wa sekta ya fedha na uchumi mkuu kama kichochea muhimu cha upatikanaji wa fedha na mitaji," anasema Gavana.

Mpango huo pia unaweka malengo ya kuongeza mikopo kwa sekta binafsi, kuimarisha mtaji wa taasisi za fedha na kupunguza mikopo chechefu. Benki Kuu inalenga uwiano wa utoshelevu wa mtaji wa taasisi za fedha kufikia zaidi ya asilimia 16.5 na mikopo chechefu kubaki chini ya asilimia tano.

Ujumuishaji wa kifedha

Kwa upande mwingine, Benki Kuu imeweka ujumuishaji wa kifedha kuwa sehemu muhimu ya utekelezaji wa Dira 2050. Lengo ni kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata na kutumia huduma rasmi za kifedha.

Mikakati hiyo inahusisha kuongeza matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali, kuimarisha elimu ya fedha, kupunguza mikopo isiyolipika na kuongeza idadi ya watu wazima wanaotumia huduma rasmi za kifedha.

Gavana anaongeza kuwa Benki Kuu itaendelea kuimarisha mifumo ya malipo ili kurahisisha miamala na kupunguza utegemezi wa fedha taslimu.

"Kukuza utumiaji wa mifumo ya malipo ya kidijitali na uhamishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki kutasaidia kuongeza ufanisi, uwazi na upatikanaji wa huduma za kifedha," anasema.

Mpango wa Benki Kuu unaonyesha kuwa kiwango cha ujumuishwaji wa kifedha kwa watu wazima kinatarajiwa kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2030/31, huku upatikanaji rasmi wa huduma za kifedha ukifikia angalau asilimia 96.

Teknolojia na ubunifu

Katika dunia inayobadilika kwa kasi kutokana na teknolojia, Benki Kuu pia imeweka mkazo katika uchumi wa kidijitali, matumizi ya Akili Unde (AI), ubunifu wa kifedha na usalama wa mtandao.

"Benki Kuu itaongeza matumizi ya Akili Unde, ubunifu wa kidijitali na teknolojia nyingine zinazoibukia katika kuongeza ufanisi wa shughuli za utoaji huduma za Benki," anaeleza Gavana.

Hatua hizo zinalenga kuhakikisha mifumo ya fedha inakuwa salama, yenye ufanisi na inayoweza kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia.

Kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

Benki Kuu pia imeingiza masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango yake ya muda mrefu. Hii ni pamoja na kuimarisha ustahimilivu wa sekta ya fedha dhidi ya athari za ukame, mafuriko na matukio mengine ya hali ya hewa.

Gavana Tutuba anasema Benki Kuu inalenga kuanzisha kanzidata ya takwimu za tabianchi na zana za kuchambua athari za mabadiliko hayo katika sekta ya fedha.

"Tutaimarisha ustahimilivu kuhusiana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kutekeleza taksonomia ya fedha na uchumi wa kijani," amesema.

Wananchi kupima mafanikio

Kwa mujibu wa mpango huo, utekelezaji wa Dira 2050 hautaishia kwenye mipango pekee, bali utapimwa kupitia viashiria mahsusi vya uchumi na sekta ya fedha.

Miongoni mwa viashiria hivyo ni mfumuko wa bei, ukuaji wa Pato la Taifa, akiba ya fedha za kigeni, mikopo kwa sekta binafsi, amana za benki, kiwango cha mikopo chechefu, ujumuishaji wa kifedha na matumizi ya malipo ya kidijitali.

"Benki Kuu huoanisha mpango mkakati wake wa miaka mitano na vipaumbele vya kitaifa na kuangalia mafanikio ya viashiria maalumu vya sekta ya fedha na uchumi mkuu ili kuchangia mafanikio ya malengo ya Dira ya 2050," amesema Gavana.

Kwa mtazamo huo, mchango wa Benki Kuu katika Dira 2050 utaonekana si katika sera pekee, bali pia katika mazingira ya uchumi ambayo yanamwezesha mwananchi, mfanyabiashara, mwekezaji na mzalishaji kufanya shughuli zao kwa uhakika zaidi.





Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba (kulia), katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ni Dkt. Bill Kiwia(kushoto), katika picha ya pamoja baada ya uzinduzi wa Mwongozo wa Utoaji Ufadhili kwa Wanafunzi Wanufaika wa Mfuko wa Ufadhili wa Mwl. Julius Nyerere uliofanyika jijini Dar es Salaam.

BoT YAIKABIDHI HESLB JUKUMU LA KURATIBU UPATIKANAJI WANUFAIKA WA MFUKO WA MWALIMU NYERERE

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imeikabidhi Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) jukumu la kusimamia mchakato wa maombi ya wanufaika wa Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (Mwalimu Nyerere Memorial Scholarship Fund), hatua inayolenga kuongeza uwazi, usawa na ufanisi katika utoaji wa ufadhili kwa wanufaika wa elimu ya juu nchini.

Uamuzi huo umeanza kutumika katika udahili wa mwaka wa masomo 2026/27 baada ya Bodi ya Usimamizi wa Mfuko huo kuridhia kutumia mifumo ya HESLB katika mchakato wa kutangaza, kupokea na kuchakata maombi ya wanafunzi wanaostahili kupata ufadhili.

Hayo yamesemwa Agosti 28,2026 jijini Dar es Salaam na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba wakati akizindua mwongozo mpya wa utoaji ufadhili kwa wanafunzi wanaonufaika na Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Gavana Tutuba amesema, uamuzi huo ulifikiwa na Bodi ya Mfuko katika kikao chake kilichofanyika Mei,mwaka huu, baada ya kubaini umuhimu wa kutumia mifumo iliyopo serikalini ili kurahisisha mchakato wa kuwapata wanafunzi wenye sifa.

Amesema hapo awali, tangu mfuko huo ulipoanzishwa mwaka 2009, nafasi za ufadhili zilitangazwa kupitia vyombo vya habari, vikiwamo televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii, ambapo wanafunzi wenye sifa waliwasilisha maombi yao na kuchambuliwa na timu ya wataalamu wa BoT.

“Tumekubaliana sasa kutumia mifumo inayoratibiwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mfumo huo una uwezo wa kutumia taarifa za ufaulu kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), hivyo kutuwezesha kupata wanafunzi wenye sifa kwa utaratibu wenye ufanisi zaidi,” amesema Gavana Tutuba.

Amesema,mabadiliko hayo yanaendana na msisitizo wa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu umuhimu wa mifumo ya Serikali kusomana ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Gavana huyo, badala ya kuendelea na utaratibu wa kutangaza nafasi na kusubiri maombi, HESLB itaweza kutumia mifumo yake iliyopo kuchakata taarifa za wanafunzi na kubaini wanaokidhi vigezo vya ufadhili.

“Kwa kuwa mfumo wa Bodi ya Mikopo tayari unachakata taarifa za wanafunzi na kubaini wanaostahili kupata mikopo, tumeona ni jambo jema kutumia utaratibu huo huo katika kupata wanufaika wa Mfuko wa Mwalimu Nyerere,” amesema

Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ulianzishwa Oktoba 12, 2009 ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuenzi mchango wa Baba wa Taifa katika kuendeleza elimu na rasilimali watu nchini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt.Bill Kiwia amesema, jukumu la kusimamia mchakato wa ufadhili huo ni heshima kubwa kwa taasisi hiyo na ni ishara ya imani iliyowekwa na BoT katika uwezo wa HESLB.

Dkt.Kiwia amesema, ushirikiano huo unaonesha namna taasisi za Serikali zinavyoweza kutumia mifumo na uwezo wao kwa pamoja ili kuboresha huduma kwa Watanzania.

“Leo historia inaandikwa. Bodi ya Mikopo imekabidhiwa jukumu la kutangaza na kupokea maombi ya ufadhili kwa ajili ya vijana wetu wa Kitanzania,”amesema.

Amesema,HESLB imewekeza zaidi ya dola milioni tano katika kujenga na kuimarisha mifumo yake ya kidijitali inayowezesha usimamizi wa mchakato mzima wa mikopo na ufadhili wa wanafunzi.

Miongoni mwa mifumo hiyo ni Mfumo wa Usimamizi wa Maombi Mtandaoni (OLAMS), unaotumika kupokea na kuchakata maombi ya wanafunzi.

Dkt.Kiwia amesema,mfumo mwingine ni Integrated Loan Management System (ILMS), unaowezesha kufuatilia mwanafunzi kuanzia anapoanza masomo, anapoendelea na masomo hadi anapohitimu na kuanza kurejesha mkopo.

Amesema,HESLB pia imejenga mfumo wa kidijitali wa utoaji fedha kwa wanufaika pamoja na mfumo wa malipo ya marejesho unaounganishwa na Serikali e-Payment Gateway (GePG).

Pia,amesema taasisi hiyo imefikia kiwango cha takribani asilimia 98 cha matumizi ya mifumo isiyohitaji karatasi katika shughuli zake, jambo linalorahisisha utunzaji wa nyaraka na uchakataji wa taarifa.

Dkt.Kiwia amesema,HESLB imewezesha zaidi ya Watanzania milioni moja kupata elimu ya juu kupitia mikopo, huku zaidi ya Shilingi trilioni 9 zikitolewa kwa wanufaika.

Amesema,bodi hiyo pia imeendelea kusimamia programu nyingine za ufadhili, ikiwemo Samia Scholarship ambayo tangu ilipoanzishwa mwaka 2022 imewanufaisha zaidi ya wanafunzi 2,000 katika fani za Sayansi, Tiba, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

TAKWIMU: UCHUMI WA TANZANIA WAENDELEA KUWA STAHIMILIVU



Licha ya misukosuko inayoendelea duniani ikiwemo vita za Mashariki ya Kati pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta, bado viasharia vinaonesha uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa stahimilivu.

Kwa muktadha wa kiuchumi, viashiria hivyo ni pamoja na; Utulivu wa bei, ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, kuimarika kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi pamoja na kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni.

Mfumuko wa bei wabaki ndani ya malengo

Moja ya viashiria vinavyotumika kupima uimara wa uchumi ni mwenendo wa mfumuko wa bei. Tanzania iliendelea kuwa na mfumuko wa bei uliodhibitiwa katika kipindi hicho.

Takwimu za Ripoti ya Tathmini ya Uchumi Agosti 2026 zinaonesha kuwa mfumuko wa bei wa jumla ulifikia asilimia 4.2 Julai 2026, kutoka asilimia 4.0 Juni mwaka huo.

"Pamoja na ongezeko hilo, kiwango hicho kiliendelea kuwa ndani ya lengo la taifa na vigezo vya mtangamano vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

"Mwenendo huo unaonesha kuwa, kwa ujumla, nguvu ya kupanda kwa bei imeendelea kudhibitika, hali inayosaidia kulinda uwezo wa wananchi na wafanyabiashara kupanga matumizi na uwekezaji kwa mazingira yenye utabiri zaidi," imeeleza ripoti hiyo.

Ripoti hiyo inaonesha kuwa Kwa upande wa chakula, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.1, kutoka asilimia 7.6 mwaka mmoja uliopita. Ripoti imeeleza kuwa hali hiyo ilisaidiwa na kuongezeka kwa upatikanaji wa chakula wakati wa mavuno.

Uimarishaji wa upatikanaji wa chakula umeendelea kuwa jambo muhimu katika kudhibiti shinikizo la bei, hasa kwa kuwa chakula kina uzito mkubwa katika matumizi ya kaya.

"Akiba ya chakula iliyokuwa imehifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilifikia tani 479,065 mwishoni mwa Julai 2026, zaidi ya mara tatu ya kigezo cha kitaifa cha angalau tani 150,000. Licha ya misukosuko ya uchumi wa dunia, Tanzania iliendelea kudumisha utulivu wa bei," imeeleza Ripoti ya Tathmini ya Uchumi ya Agosti 2026.

Sera ya fedha yaendelea kujibu changamoto

Katika kudhibiti mfumuko wa bei unaoweza kujitokeza, Kamati ya Sera ya Fedha iliongeza Riba ya Benki Kuu kutoka asilimia 5.75 ya robo mwaka ulioishia Julai hadi asilimia 6.25 kwa robo mwaka uliyoishia Septemba 2026.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Tathmini ya Uchumi ya Agosti 2026, hatua hiyo ililenga kukabili shinikizo la mfumuko wa bei lililoanza kujitokeza, likiwamo uwezekano wa athari za awamu ya pili zinazoweza kutokana na gharama kubwa za nishati, mbolea na usafirishaji kutoka nje.

Mikopo sekta binafsi yakua kwa kasi

Pamoja na hatua za kuimarisha utulivu wa bei, upatikanaji wa fedha kwa sekta binafsi umeendelea kukua na kuimarika.

Ripoti hiyo inaonesha kuwa mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 31.2 Julai 2026, kutoka asilimia 28.1 Juni 2026. Ukuaji huo ulienda sambamba na kupanuka kwa shughuli za uchumi na mahitaji ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mazao.

Takwimu zinaonyesha kuwa sekta mbalimbali za uzalishaji zilinufaika na ongezeko hilo la mikopo. Uchukuzi na mawasiliano uliendelea kuongoza kwa ukuaji wa mikopo wa asilimia 66.0, ukifuatiwa na uchimbaji madini kwa asilimia 65.2, biashara (asilimia 43.5), ujenzi (asilimia 38.9) na kilimo (asilimia 37.3), sekta ya hoteli na migahawa (asilimia 25.1).

Kwa mujibu wa Ripoti ya Tathmini ya Uchumi ya Agosti 2026, ukuaji wa mikopo unaonesha kuwa shughuli za uzalishaji zinaendelea kuhitaji mitaji, hali inayoweza kusaidia kuendeleza biashara, uwekezaji na ajira.

Mauzo nje yaongezeka

Sekta ya nje nayo imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha uchumi na upatikanaji wa fedha za kigeni. Katika mwaka ulioishia Julai 2026, mauzo ya bidhaa na huduma nje yaliongezeka kwa asilimia 16.5 na kufikia dola za Marekani milioni 19,985.8. Mauzo ya bidhaa pekee yaliongezeka kwa asilimia 20.7 hadi dola milioni 11,951.7.
Dhahabu iliendelea kuwa kinara wa mapato hayo, huku mauzo yake yakiongezeka kwa asilimia 37.4 hadi dola milioni 5,670.7, sawa na asilimia 47.4 ya mapato yote ya mauzo ya bidhaa nje.

Bidhaa za viwandani ziliongeza mapato yake kwa asilimia 46.0 hadi dola milioni 2,215.5, wakati mazao ya asili yaliongezeka kwa asilimia 14.9 hadi dola milioni 1,628.8, yakiongozwa na tumbaku na kahawa.

"Ongezeko la mapato ya dhahabu, bidhaa za viwandani, mazao ya biashara, usafirishaji na utalii linaonesha nafasi ya kupanua masoko," imeeleza Ripoti ya Tathmini ya Uchumi ya Agosti 2026.

Utalii na usafirishaji waendelea kuingiza fedha

Mbali na bidhaa, huduma zimeendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato ya fedha za kigeni.

Mapato ya huduma yalifikia dola milioni 8,034.1, yakichangiwa na utalii na usafirishaji wa bidhaa. Mapato ya huduma za usafirishaji yalikua kwa asilimia 29.7 hadi dola milioni 3,221.5 kutokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa mizigo inayovuka mipaka.

Kwa upande wa utalii, mapato yalifikia dola milioni 4,292.8. Mwenendo huo unaonesha kuongezeka kwa nafasi ya sekta ya huduma katika uchumi, huku Tanzania ikiendelea kunufaika na utalii pamoja na nafasi yake katika shughuli za usafirishaji wa mizigo katika ukanda wa Afrika Mashariki na maeneo mengine.

Akiba ya fedha za kigeni yaongezeka

Uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni ni miongoni mwa nguzo muhimu za ustahimilivu wa uchumi kwa sababu huwezesha nchi kukidhi mahitaji ya uagizaji na kupunguza shinikizo kwenye soko la fedha za kigeni.

Hadi mwishoni mwa Julai 2026, akiba ghafi ya fedha za kigeni ilifikia dola milioni 6,199.6, sawa na uwezo wa kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.8.

Wakati huo huo, soko la fedha za kigeni liliendelea kuwa tulivu kwa ujumla kutokana na uwepo wa ukwasi wa kutosha wa fedha za kigeni, ukichangiwa na mauzo ya dhahabu, mazao ya asili na shughuli za utalii.

Mauzo katika soko la fedha za kigeni baina ya mabenki yaliongezeka hadi dola milioni 227.1 Julai 2026 kutoka dola milioni 193.3 Juni. Benki Kuu iliuza dola milioni 110.3 ili kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi.


Shilingi ilipungua thamani kwa asilimia 0.8 kwa mwezi hadi wastani wa Sh2,653.52 kwa dola, lakini iliimarika kwa asilimia 0.5 kwa mwaka.

Mapato ya Serikali yazidi lengo

Mwenendo chanya umeonekana pia katika upande wa mapato ya Serikali. Mapato yaliyokusanywa Juni 2026 yalifikia TZS 4,658.2 bilioni, ambayo ni asilimia 5.4 zaidi ya lengo. Katika mapato hayo, makusanyo ya kodi yalifikia TZS 3,733.2 bilioni, asilimia 12.5 juu ya lengo.

Kwa wafanyabiashara na wawekezaji, mwenendo huo unaweza kuashiria uwezo mkubwa zaidi wa Serikali kugharamia shughuli zake na kuendelea kutekeleza mipango ya maendeleo, huku mapato ya ndani yakiendelea kuwa sehemu muhimu ya usimamizi wa uchumi.

SEKTA YA BENKI INAVYOCHOCHEA UCHUMI NCHINI



Sekta ya benki nchini Tanzania imeendelea kuwa nguzo muhimu ya uchumi kwa kuchochea uwekezaji, biashara na uzalishaji kupitia ukusanyaji wa amana, utoaji wa mikopo na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi na wafanyabiashara.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha Benki Kuu ya Tanzania (BoT), sekta ya fedha kwa ujumla ina nafasi muhimu katika kusaidia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii, huku sekta ya kibenki ikiwa nguzo kuu kwa kuwa inachangia zaidi ya asilimia 70 ya mali zote za sekta ya fedha.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa mchango wa sekta ya benki hauishii katika kuhifadhi fedha za wananchi, bali unahusisha pia kuhamasisha rasilimali za kifedha, kufadhili uwekezaji na shughuli za uzalishaji, kukuza ujumuishi wa kifedha na kusaidia ustawi wa uchumi kwa ujumla.

Hadi Agosti 31, 2026, sekta ya kibenki nchini ilikuwa na taasisi 44 zilizokuwa zikitoa huduma za kibenki. Kati ya hizo, 35 zilikuwa benki za biashara, tano benki zinazotoa huduma ndogo za kifedha, mbili benki za jamii na mbili benki za maendeleo.

Pamoja na taasisi hizo, sekta ya huduma ndogondogo za fedha imeendelea kupanuka, ikiwa na taasisi za mikopo pekee 3,229, vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) 1,030 na vikundi vya kijamii 81,878 vinavyotoa huduma za kifedha katika ngazi ya jamii.

“Sekta ya fedha nchini inaendelea kuwa mhimili muhimu katika kusaidia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii,” imeeleza taarifa ya Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha Benki Kuu ya Tanzania.

Mikopo ya Sh57 trilioni

Moja ya njia kuu ambayo sekta ya benki inachochea uchumi ni kupitia utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi Juni 2026, thamani ya mikopo, dhamana za mikopo na akaunti za kuruhusu kutoa zaidi ya salio ilifikia TZS 57.09 trilioni.

Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 32.27 kutoka TZS 43.16 trilioni zilizotolewa katika kipindi kilichoishia Juni 2025.

Ukuaji huo unaonyesha nafasi inayoongezeka ya taasisi za benki katika kufadhili shughuli za kiuchumi zinazohitaji mitaji kwa ajili ya kuanzisha, kupanua au kuendeleza biashara na uzalishaji.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mikopo hiyo ilielekezwa zaidi katika sekta za biashara, viwanda, kilimo, ujenzi, mawasiliano pamoja na usafirishaji.

“Ukuaji huu unaashiria kuendelea kwa mchango wa sekta ya benki katika kufadhili shughuli za kiuchumi na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa sekta mbalimbali za uzalishaji, biashara na huduma,” imeeleza taarifa ya Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa mtazamo huo, mikopo ya benki ina nafasi kubwa katika kuongeza uzalishaji, uwekezaji, biashara na ajira, mambo ambayo kwa pamoja yanaweza kuongeza mzunguko wa shughuli za kiuchumi nchini.

Hii ina maana kuwa benki zinapoongeza uwezo wa kutoa mikopo yenye masharti yanayozingatia mazingira ya soko, mitaji huingia katika maeneo ya uzalishaji na biashara, hivyo kuleta shughuli zaidi za kiuchumi.

Ujumuishi wa kifedha wapewa nguvu

Mchango mwingine wa sekta ya benki ni kupanua upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi waliokuwa wakikosa huduma hizo kwa urahisi, hasa maeneo ya vijijini na makundi ya kipato cha chini.

Hadi Agosti 31, 2026, sekta hiyo ilikuwa na matawi 1,095 na mawakala wa benki 201,045 katika maeneo mbalimbali nchini.

Dar es Salaam ndiyo mkoa uliokuwa na matawi mengi zaidi, ukiwa na matawi 280 sawa na asilimia 26 ya matawi yote nchini. Mwanza (matawi 72), Arusha (71), Dodoma (52) na Kilimanjaro (48).

Kwa mtazamo wa taarifa hiyo, kuongezeka kwa matawi na mawakala wa benki kunarahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha na hivyo kuchochea shughuli za biashara na uchumi katika maeneo mbalimbali.
Kwa upande mwingine, ongezeko la SACCOS, taasisi za mikopo na vikundi vya kijamii linaonyesha kuwa mfumo wa fedha unazidi kusogea karibu na wananchi, hususan wale wanaohitaji huduma ndogo za kifedha katika ngazi ya jamii.

Hali hiyo ni muhimu katika kuongeza uwezo wa wananchi kuweka akiba, kupata mikopo na kutumia huduma rasmi za kifedha katika shughuli zao za kila siku.

Ikumbukwe pia, katika suala la ujumuishi Tanzania kupitia BoT, imetambulika kimataisha na kupewa tuzo ya kufanya vizuri katika eneo hilo na Jumuiya ya Huduma Jumuishi za Fedha (AFI).

BoT ilipata tuzo hiyo ya Azimio la Maya (Maya Declaration Award) iliyotolewa Septemba 2026, kutokana na maendeleo katika kutekeleza ahadi zake za kuendeleza huduma jumuishi za fedha.

Mitaji na ukwasi wakutosha

Uwezo wa sekta ya benki kuchochea uchumi unategemea pia uimara wake. Taarifa ya Benki Kuu inaonyesha kuwa hadi Agosti 31, 2026, sekta ya kibenki iliendelea kuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha pamoja na kuendelea kupata faida.


Kiwango cha mtaji mkuu wa sekta hiyo kilikuwa asilimia 17.86, juu ya kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10, wakati mtaji jumla ulikuwa asilimia 19.16 dhidi ya kiwango cha chini cha asilimia 12.

“Takwimu hizi zinaonyesha uimara wa sekta na uwezo wake wa kuhimili changamoto mbalimbali,” imeeleza taarifa ya Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa upande wa ukwasi, sekta hiyo ilikuwa na kiwango cha asilimia 26.05, ikiwa juu ya kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 20.

Hii inaonyesha kuwa benki zilikuwa na uwezo wa kutosha wa kutimiza mahitaji ya wateja ya kutoa fedha na kutekeleza majukumu yao ya kifedha kwa wakati.

“Uwezo huu unaendelea kudumisha uthabiti na kuimarisha imani ya umma katika mfumo wa kifedha,” imeeleza taarifa hiyo.



Faida za benki zaongezeka

Katika kipindi kilichoishia Juni 2026, sekta ya benki ilipata faida baada ya kodi, ambayo haikuwa imekaguliwa, ya TZS 2.69 trilioni, ikilinganishwa na TZS 2.40 trilioni zilizorekodiwa katika kipindi hadi Juni 2025.

Aidha, hadi Agosti 2026, faida kwa mali (ROA) ilikuwa asilimia 4.68 huku faida kwa mtaji wa wanahisa (ROE) ikiwa asilimia 22.26.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha BoT, mwenendo huo unaonyesha uwezo wa sekta ya benki kuzalisha mapato kutoka vyanzo mbalimbali na kuendelea kuimarisha uwezo wake wa kifedha.

Wakati huohuo, ubora wa mikopo uliendelea kuwa wa kuridhisha, huku kiwango cha mikopo chechefu kikiwa asilimia 2.50, chini ya kiwango cha juu kinachokubalika cha asilimia tano.

Hali hiyo inaonyesha kuwa benki zimeendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa hatari za mikopo, tathmini ya wakopaji na ufuatiliaji wa marejesho, jambo linalosaidia kulinda afya ya sekta ya fedha.

Teknolojia yabadilisha huduma

Teknolojia nayo imekuwa sehemu muhimu ya mabadiliko katika sekta ya benki. Benki zimeendelea kutumia majukwaa ya kidijitali, huduma za benki kwa njia ya simu za mkononi, akili unde na mifumo ya kuhifadhi na kuchakata taarifa kupitia mtandao.

Mabadiliko hayo yamefanya huduma za benki kuwa rahisi zaidi, za haraka na zenye ufanisi mkubwa, huku yakipanua wigo wa wananchi wanaoweza kutumia huduma za kifedha.

“Teknolojia mbalimbali zimebadili namna huduma za kibenki zinavyotolewa na kufanya huduma hizo kupatikana kwa urahisi zaidi, kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa,” imeeleza taarifa ya Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha Benki Kuu ya Tanzania.

Hata hivyo, ukuaji wa huduma za kidijitali unaambatana na changamoto zinazohitaji usimamizi wa karibu. Miongoni mwa changamoto hizo ni hatari za usalama wa mtandao, faragha na ulinzi wa taarifa za wateja pamoja na hatari za kiutendaji na mifumo ya teknolojia.

Kwa hiyo, maendeleo ya kidijitali yanahitaji kwenda sambamba na uimarishaji wa mifumo ya udhibiti wa hatari ili kuhakikisha ubunifu hauathiri uthabiti wa mfumo wa fedha wala usalama wa watumiaji wa huduma.

Mchango, Uimara, na Ukuaji wa Sekta ya Benki Tanzania




Mchango wa 70%+ Kwenye Sekta ya Fedha

Benki zinalinda na kumiliki zaidi ya asilimia 70 ya mali zote za fedha nchini.


Mikopo Imefikia TZS 57.09 Trilioni

Ongezeko la asilimia 32.27 la mikopo kwa sekta binafsi kufikia Juni 2026.





Faida Baada ya Kodi Yafika TZS 2.69 Trilioni




Jumla ya Taasisi 44 za Kibenki

- Benki za Biashara 35
- Huduma Ndogo 5
- Jamii 2
- Maendeleo 2

Matawi 1,095 na Mawakala 201,045

Mtandao mpana wa huduma unaoongeza ujumuishi wa kifedha nchini kote.

Mikoa Inayoongoza kwa Matawi



Imara | Inakua | Jumuishi | Inaunga Mkono Uchumi

KARIBIA NUSU YA MAUZO YA BIDHAA NJE 2025/2026 YACHANGIWA NA DHAHABU



Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yameendelea kuimarika, huku dhahabu ikichangia karibu nusu ya mapato yote yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje, kwa mujibu wa takwimu za uchumi za mwaka wa fedha 2025/2026.

Kwa mujibu wa takwimu hizo zilizotokana na Ripoti ya Tathmini ya Uchumi ya Agosti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 16.5 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025.

Takwimu zinaonesha kuwa mwaka wa fedha 2024/2025 mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa Dola za Marekani milioni 16,688.14 ambapo mwaka wa fedha 2025/2026 yaliongezeka na kufikia Dola za Marekani milioni 19,985.8.

"Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuimarika kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma, hususan usafirishaji,"imeeleza ripoti hiyo.

Dhahabu yaongoza

Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 20.7 na kufikia Dola za Marekani milioni 11,951.7, kutoka kiwango cha mwaka uliotangulia.

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 dhahabu ilikuwa kinara ambapo mauzo yake yalifikia Dola za Marekani milioni 5,670.7, kutoka Dola milioni 4,127.1 mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la takribani asilimia 37.4.

Ripoti hiyo inataja ongezeko hilo lilichangiwa na bei nzuri ya dhahabu katika soko la dunia, hali iliyoongeza thamani ya mauzo ya madini hayo.

Kwa kiwango hicho, dhahabu ilichangia takribani asilimia 47.4 ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi, ikimaanisha kuwa karibu dola moja kati ya kila dola mbili zilizopatikana kutokana na mauzo ya bidhaa nje ilitokana na dhahabu ambayo ni karibu nusu ya mauzo yote.

Viwanda vyapiga hatua

Mbali na dhahabu, bidhaa za viwandani nazo zilionyesha ongezeko kubwa katika kipindi hicho.

Takwimu zinaonesha kuwa mauzo ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kwa asilimia 46.0, kutoka dola milioni 1,517.3 mwaka 2025 hadi dola milioni 2,215.5 mwaka 2026.

Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za chuma na bidhaa zake, bidhaa za kioo pamoja na nguo.

Ukuaji huo unaonesha pia kuendelea kwa mahitaji ya bidhaa zinazozalishwa nchini katika masoko ya kikanda.

Tumbaku na kahawa

Katika kundi la bidhaa za asilia, mauzo yaliongezeka kwa asilimia 14.9 na kufikia Dola milioni 1,628.8. Ripoti imeyataja mazao ya tumbaku na kahawa kuwa miongoni mwa bidhaa zilizochangia ongezeko hilo.

Kwa upande wa tumbaku pekee, mauzo yaliongezeka kutoka Dola milioni 443.0 mwaka 2024/2025 hadi Dola milioni 588.6 mwaka 2025/2026 nayo kutoka Dola milioni 337.5 hadi Dola milioni 396.0 katika kipindi hicho.

Usafirishaji nao waimarika

Huduma za usafirishaji ziliendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato ya Tanzania kutoka nje ya nchi. Mapato yatokanayo na huduma hizo yaliongezeka kutoka Dola milioni 2,555.5 mwaka 2024/2025 hadi Dola milioni 3,221.5 mwaka 2025/2026.

Ripoti imeeleza ongezeko hilo linaashiria kuongezeka kwa shughuli zinazohusiana na usafirishaji wa mizigo na huduma nyingine za usafiri, sambamba na kuongezeka kwa shughuli za biashara

Uagizaji nao wapanda

Wakati mauzo ya nje yakiongezeka, upande wa uagizaji wa bidhaa nao uliongezeka kwa asilimia 18.3 mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka 2024/2025.

"Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka kutoka Dola milioni 16,999.65 mwaka 2024/2025 na kufikia Dola milioni 20,807.4 mwaka wa fedha 2025/2026,"imeeleza ripoti hiyo.

Kuhusu sababu la kuongezeka kwa uagizaji, ripoti hiyo imeeleza; "Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa mtaji, bidhaa za viwandani, mafuta ya petroli pamoja na huduma za usafirishaji wa mizigo."

Uagizaji wa bidhaa pekee ulifikia Dola milioni 17,439.3 mwaka wa fedha 2025/2026, kutoka Dola milioni 14,421.3 mwaka 2024/2025.

Bidhaa mtaji na bidhaa za kati zilitajwa kuwa miongoni mwa zilizochangia ongezeko hilo, hali inayoendana na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji na uzalishaji viwandani.

Kwa ujumla, takwimu hizo zinaonesha kuongezeka kwa shughuli za biashara ya nje ya Tanzania, huku dhahabu ikiendelea kuwa bidhaa yenye mchango mkubwa katika mapato ya mauzo ya nje, sambamba na kuimarika kwa mauzo ya bidhaa za viwandani, tumbaku, kahawa na huduma za usafirishaji.

Dhahabu: Kinara wa Mauzo ya Bidhaa Nje ya Nchi Tanzania (2025/2026)

Karibu nusu ya mapato yote ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi.

Dola Milioni 5,670.7 Zilizopatikana

Ongezeko la asilimia 37.4 kutoka Dola milioni 4,127.1 mwaka 2024/2025.



47.4%

ya Mapato Yote ya Bidhaa

Karibu nusu ya mauzo yote ya bidhaa nje yalitokana na dhahabu.

Bei Nzuri Katika Soko la Dunia

Kuimarika kwa bei ya dhahabu kimataifa kumeongeza thamani ya mauzo.

Ulinganisho wa Dhahabu na Sekta Nyingine

	Mapato (USD Milioni)	Ukuaji
Dhahabu	5,670.7	+37.4%
Bidhaa za Viwandani	2,215.5	+46.0%
Mazao ya Asili (Tumbaku, Kahawa n.k.)	1,628.8	+14.9%

Dhahabu Yaongoza kwa Thamani Kubwa

Mapato ya dhahabu yamezidi kwa mbali bidhaa za viwandani na mazao ya asili.



HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA ZAING'ARISHA BoT KIMATAIFA

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ilitambuliwa miongoni mwa taasisi tatu bora kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Huduma Jumuishi za Fedha (Alliance for Financial Inclusion – AFI) duniani, kutokana na uongozi madhubuti katika sera za huduma jumuishi za fedha na juhudi za kupunguza pengo la kijinsia katika upatikanaji wa huduma za fedha.

Utambuzi huo ulitolewa kupitia vipengele mbalimbali vya tuzo na vyeti vya AFI, ikiwemo Tuzo ya Azimio la Maya (Maya Declaration Award), inayotambua mafanikio ya nchi katika kuweka, kupima na kutekeleza ahadi za kuendeleza huduma jumuishi za fedha.

Benki Kuu pia ilitambuliwa kwa nafasi yake katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Denarau (Denarau Action Plan), ambao unaweka msisitizo katika kuendeleza huduma jumuishi za fedha kwa wanawake na kuchukua hatua madhubuti za kupunguza pengo la kijinsia katika huduma za fedha. Aidha, Benki ilitambuliwa kwa juhudi za kuandaa na kutekeleza sera mbalimbali zinazochangia kupunguza pengo hilo.

Vyeti hivyo vya kutambuliwa vilipokelewa na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, wakati wa Jukwaa la Kimataifa la Sera za Huduma Jumuishi za Fedha la mwaka 2026, lililofanyika Port Moresby, Papua New Guinea, kuanzia tarehe 1 hadi 4 Septemba 2026.

Akizungumza katika mjadala uliobeba mada kuhusu "Afya ya Kifedha: Msingi wa Uchumi Himilivu na Mustakabali Jumuishi.", Gavana Tutuba alieleza uzoefu na maendeleo ya Tanzania katika kuimarisha afya ya kifedha kupitia mfumo unganishi wa malipo ya kidijitali, sera na mikakati ya maendeleo ya sekta ya fedha, pamoja na programu za elimu na uwezo wa kifedha.

Aidha, alisisitiza kuwa upatikanaji wa huduma za fedha ni hatua ya mwanzo, na kwamba matokeo halisi yanapaswa kuonekana katika uwezo wa wananchi kusimamia mapato na matumizi yao, kuweka akiba, kutumia mikopo kwa tija, kukabiliana na misukosuko ya kifedha na kuboresha maisha yao.

Pia, Gavana Tutuba alipewa heshima ya kukabidhi Tuzo ya Ubunifu katika Huduma Jumuishi za Fedha ya Nestor Espenilla Jr. ya mwaka 2026 kwa Benki Kuu ya Zambia, iliyotwaa tuzo hiyo.

Jukwaa hilo liliandaliwa na Jumuiya ya Huduma Jumuishi za Fedha (AFI), inayojumuisha taasisi wanachama kutoka nchi 84, na lilihudhuriwa na zaidi ya washiriki 700 kutoka nchi 79.

Mafanikio hayo yanaakisi hatua zinazotekelezwa na Benki Kuu katika kuimarisha mazingira ya kisera na kiudhibiti, kukuza matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma za fedha, kupunguza pengo la kijinsia na kuhakikisha huduma rasmi za fedha zinawafikia na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi.

Pia yanaonesha maendeleo ya Tanzania katika kutekeleza ahadi za Azimio la Maya, linalohimiza taasisi wanachama wa AFI kuweka na kutekeleza malengo mahsusi na yanayopimika ya kuongeza upatikanaji na matumizi ya huduma jumuishi za fedha, pamoja na kupunguza pengo la kijinsia.

Katika hatua nyingine, Meneja wa Idara ya Huduma Jumuishi za Fedha, Bi. Nangi Massawe, alitunukiwa cheti cha utambuzi katika kipengele cha Uongozi wa Sera za Huduma Jumuishi za Fedha, huku Meneja wa Idara ya Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha, Dkt. Khadijah Kishimba, akitambuliwa katika kipengele cha Mwenendo wa Soko na Uwezeshaji wa Watumiaji wa Huduma za Fedha.

Vilevile, watumishi watatu wa Benki Kuu, Bw. Sadiki Nyanzowa, Bw. Thomas Mongella na Bi. Kidee Mshihiri, walihitimu Programu ya Uongozi katika Huduma Jumuishi za Fedha ya Fletcher School na kutunukiwa vyeti vya kuhitimu.

Mafanikio hayo yanaongeza uwezo wa wataalamu wa Benki Kuu katika kuongoza uandaaji na utekelezaji wa sera na mikakati ya huduma jumuishi za fedha.

Jukwaa hilo lililoongozwa na kaulimbiu ya "Uchumi Himilivu, Mustakabali Jumuishi", liliwakutanisha Magavana na Naibu Magavana wa Benki Kuu, viongozi wa mamlaka za usimamizi wa sekta ya fedha, taasisi za maendeleo, sekta binafsi, watoa huduma za teknolojia na washirika wengine kutoka nchi mbalimbali.



Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba akizungumza katika mjadala kuhusu "Afya ya Kifedha: Msingi wa Uchumi Himilivu na Mustakabali Jumuishi.", uliofanyika katika Jukwaa la Kimataifa la Sera za Huduma Jumuishi za Fedha la mwaka 2026, lililofanyika Port Moresby, Papua New Guinea, kuanzia tarehe 1 hadi 4 Septemba 2026.

BoT YATAMBULIWA KIMATAIFA KWA MAFANIKIO YA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA



Meneja wa Idara ya Huduma Jumuishi za Fedha, Bi. Nangi Massawe, akionyesha Tuzo ya Kinara wa AFI katika Huduma Jumuishi za Fedha kwa Jinsia katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika BoT jijini Dar es Salaam tarehe 16 Septemba 2026.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetambuliwa kimataifa kwa mafanikio yake katika kuendeleza na kutekeleza sera na mipango ya huduma jumuishi za fedha, baada ya kutajwa miongoni mwa taasisi wanachama zilizofanya vizuri katika vipengele mbalimbali vya Tuzo za Jumuiya ya Huduma Jumuishi za Fedha (AFI).

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika BoT jijini Dar es Salaam Septemba 16, 2026, Meneja wa Idara ya Huduma Jumuishi za Fedha, Bi. Nangi Massawe, amesema utambuzi huo umetolewa wakati wa Mkutano Mkuu wa Sera wa AFI wa mwaka 2026 (AFI Global Policy Forum – GPF 2026), uliofanyika Port Moresby, Papua New Guinea, kuanzia tarehe 1 hadi 4 Septemba 2026.

Bi. Massawe amesema Tanzania ilitambuliwa katika Tuzo ya Azimio la Maya (Maya Declaration Award) kutokana na maendeleo katika kutekeleza ahadi zake za kuendeleza huduma jumuishi za fedha. Tanzania imeweka jumla ya ahadi 13 chini ya Azimio hilo, ikiwemo utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa Tatu (NFIF 2023–2028).

Amesema mafanikio hayo yanaonekana pia katika kuongezeka kwa ujumuishaji rasmi wa kifedha kutoka asilimia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023, huku matumizi ya huduma za fedha kwa njia ya simu yakiongezeka kutoka asilimia 60 hadi asilimia 72 katika kipindi hicho.

Aidha, amesema Benki Kuu ilitambuliwa katika Tuzo ya Mafanikio katika Sera za Huduma Jumuishi za Fedha, (Financial Inclusion Policy Achievement Award) kwa juhudi za kuimarisha upatikanaji wa huduma za fedha kwa makundi maalumu na yaliyo katika mazingira magumu.

Katika eneo la ujumuishaji wa kifedha kwa wanawake, Tanzania ilitambuliwa pia kama taasisi kinara katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Denarau (AFI Denarau Action Plan), unaolenga kupunguza pengo la kijinsia katika huduma za fedha.

Bi. Massawe amesema utambuzi huo ni matokeo ya hatua mbalimbali za kisera, kiudhibiti na kiteknolojia zinazotekelezwa na Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya fedha, ikiwemo matumizi ya mifumo ya Tiered KYC, Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo Tanzania (TIPS) na TANQR.

Mbali na utambuzi wa taasisi, wataalamu wa Benki Kuu pia walitambuliwa katika Tuzo za Uongozi wa Kiufundi za AFI. Bi. Massawe alitambuliwa katika kipengele cha Uongozi wa Sera za Huduma Jumuishi za Fedha, huku Meneja wa Idara ya Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha, Dkt. Khadijah Kishimba, akitambuliwa katika kipengele cha Mwenendo wa Soko na Uwezeshaji wa Watumiaji wa Huduma za Fedha.

Bi. Massawe amesema Benki Kuu itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa Tatu (NFIF 2023–2028) kwa kushirikiana na Serikali, wadau wa sekta ya fedha, taasisi za maendeleo na sekta binafsi, kwa lengo la kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata na kutumia huduma rasmi za fedha.



Meneja wa Idara ya Huduma Jumuishi za Fedha, Bi. Nangi Massawe, akionyesha Tuzo ya Mafanikio katika Sera za Huduma Jumuishi za Fedha, iliyotolewa kwa BoT na Jumuiya ya Huduma Jumuishi za Fedha (AFI).



USIMAMIZI WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA TANZANIA WAIVUTIA BENKI KUU YA MALAWI

Naibu Gavana wa BoT, Bi. Sauda Msemo, akisalimiana na Naibu Gavana Benki Kuu ya Malawi, Bw. Henry Mathanga, walipokutana katika kikao cha kubadilishana uzoefu kilichofanyika jijini Dar es salaam Oktoba 12 2026.

Ujumbe kutoka Benki Kuu ya Malawi, ukiongozwa na Naibu Gavana wake, Bw. Henry Mathanga, ulitembelea Benki Kuu ya Tanzania (BoT), jijini Dar es Salaam, tarehe 12 Oktoba 2026, kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu usimamizi na udhibiti wa sekta ya huduma ndogo za fedha nchini Tanzania.

Ujumbe huo ulipokelewa na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, ambaye alieleza namna BoT inavyosimamia watoa huduma ndogo za fedha katika madaraja yote manne (Tier 1–4).

Madaraja hayo yanajumuisha taasisi za huduma ndogo za fedha zinazopokea amana, watoa huduma ndogo za fedha wasiopokea amana, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), pamoja na Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha vya Kijamii (CMGs).

Aidha, ujumbe huo ulielezwa kuwa BoT husimamia moja kwa moja watoa huduma za fedha wa Daraja la Pili, huku usimamizi wa watoa huduma wa Daraja la Tatu na la Nne ukifanyika kupitia mamlaka zilizokasimiwa majukumu hayo, ambazo ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mtawalia.

Katika kikao hicho cha kubadilishana uzoefu, pande hizo zilijadili masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa sekta ya huduma ndogo za fedha, yakiwemo ukaguzi wa watoa huduma, ufuatiliaji wa taarifa za kiusimamizi, ujenzi wa uwezo wa watoa huduma na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu ukopaji salama. Vilevile, walijadili umuhimu wa kuimarisha ushirikiano na wadau wengine wa sekta hiyo, wakiwemo vyama vinavyowakilisha watoa huduma ndogo za fedha.

Katika kuimarisha usimamizi wa sekta hiyo, BoT pia ilieleza hatua mbalimbali inazochukua kulinda watumiaji wa huduma za fedha. Hatua hizo ni pamoja na kushughulikia malalamiko ya wateja, kuchukua hatua dhidi ya watoa huduma wanaokiuka matakwa ya kisheria na udhibiti, pamoja na kuandaa na kuboresha mifumo, miongozo na taratibu zinazowezesha usimamizi wenye ufanisi.

Kwa upande wake, Bw. Mathanga alisema kuwa ziara hiyo ilitokana na kutambua juhudi na uzoefu wa Benki Kuu ya Tanzania katika kusimamia kwa ufanisi sekta ya huduma ndogo za fedha. Alieleza kuwa ziara hiyo ni fursa muhimu kwa Benki Kuu ya Malawi kujifunza mbinu na mifumo inayotumiwa na BoT ili kuboresha usimamizi wa sekta hiyo nchini Malawi.

BoT YAONYA WASANII UTUPAJI FEDHA, UKOPESHAJI HOLELA NA UPATU



Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imewaonya wananchi, wakiwemo wasanii wa fani mbalimbali kuacha tabia ya kutupa fedha chini wakati wa kutunzana katika sherehe wanazozifanya.

Pia, imewaonya kujiepusha na kufanya biashara ya ukopeshaji fedha au ukusanyaji wa amana kutoka kwa wananchi kupitia mfumo wa "upatu" au vikundi vingine visivyosajiliwa na mamlaka husika.

Onyo hilo lilitolewa Agosti 31, 2026, katika semina iliyoandaliwa na BoT kwa wasanii wa muziki na waigizaji, ikiwa na lengo la kuwajengea uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya fedha, pamoja na umuhimu wa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa katika kuendesha shughuli za kifedha.

Akifungua semina hiyo iliyofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi BoT, Dkt. Suleiman Missango, alisema wasanii ni kundi muhimu kupata elimu hiyo kutokana na ushawishi mkubwa walionao katika jamii.

Alisema ushawishi huo unawapa wasanii nafasi muhimu ya kuwaelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu uchumi na fedha, hivyo ni muhimu kuwa na uelewa sahihi ili waweze kutoa taarifa sahihi kwa jamii.

Akiwasilisha mada kuhusu Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, 2018, Mkaguzi wa Mabenki wa BoT, Bw. Joseph Lubava, alisema kwa mujibu wa Sheria hiyo, mtu au taasisi inayofanya biashara ya huduma ndogo za fedha bila kuwa na leseni halali kutoka BoT anatenda kosa la jinai.

Alisisitiza kuwa mkiukaji anaweza kukabiliwa na faini ya kati ya Shilingi milioni 20 hadi milioni 100 au kifungo cha kati ya miaka miwili hadi mitano jela, pamoja na adhabu nyingine kwa mujibu wa sheria.

Aidha, alieleza kuwa pamoja na adhabu za jinai, BoT inaweza kuchukua hatua za kiutawala dhidi ya wakiukaji, ikiwa ni pamoja na kufunga shughuli zinazofanyika kinyume cha sheria, kutaifisha mali zinazohusiana na kosa na kuorodhesha jina la mkiukaji kwa umma.

Vilevile, semina hiyo pia ilitoa elimu kuhusu utunzaji sahihi wa noti za Tanzania, ikiwemo umuhimu wa wananchi kuzitunza noti katika hali nzuri ili ziendelee kutumika kwa ufanisi katika shughuli za kiuchumi.

Wasanii wameaswa kuhakikisha wanatunza vizuri noti na sarafu ili kupunguza uharibifu wa fedha hizo na hivyo kusaidia Taifa kuepuka gharama kubwa za kuchapisha na kutengeneza noti na sarafu mara kwa mara ili kufidia zilizoharibika.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Bw. Edward Buganga, ameishukuru BoT kwa kutoa elimu hiyo kwa wasanii, ambapo amewasihi kutumia elimu waliyoipata na kuwa mabalozi wazuri wa BoT kwa kuifikisha elimu hiyo kwa jamii, hususan katika maeneo wanayofanya shughuli zao.

BoT imeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii kuhusu masuala ya fedha, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuongeza uelewa wa wananchi na kuhakikisha shughuli za kifedha zinafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.



Kaimu Katibu Mtendaji wa BASATA, Bw. Edward Bung'ang'a, akizungumza katika semina iliyoandaliwa na BoT kwa wasanii wa fani mbalimbali iliyofanyikaAgosti



Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi wa BoT, Dkt. Suleiman Missango, akizungumza katika semina ya BoT kwa wasanii iliyofanyika Agosti 31 2026, jijini Dar es Salaam.



Meneja Mawasiliano wa BoT. Bi. Victoria Msina, akizungumza katika katika semina iliyoandaliwa na BoT kwa wasanii wa fani mbalimbali iliyofanyika Agosti 31 2026.



Mwigizaji wa Filamu Nchini, Bi. Yobnesh Yusuph Hassan maarufu kama Batuli akichangia mada katika semina iliyoandaliwa na BoT kwa wasanii wa fani mbalimbali iliyofanyikaAgosti 31 2026, jijini Dar es Salaam.

ISEMAVYO SHERIA KUHUSU KUHARIBU NOTI KWA MAKUSUDI



Kitendo cha kuchana noti, kuikata, kuichora au kuiharibu kwa makusudi kinaweza kuonekana kwa baadhi ya watu kama jambo dogo linalohusu fedha wanayoimiliki wenyewe.

Hata hivyo, chini ya sheria za Tanzania, uharibifu wa makusudi wa noti halali ni kosa la jinai ambalo lina adhabu kali ya faini au kifungo jela.

Kifungu cha 332A cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Toleo la Marejeo la 2023, kinaeleza kuwa mtu ambaye bila mamlaka anaharibu, anachanachana, anakata au kwa namna nyingine anaharibu noti au fedha halali kwa makusudi anatenda kosa.

"Adhabu iliyowekwa ni faini ya TZS 500,000 kwa kila noti iliyoharibiwa au, endapo faini hiyo haitalipwa, kifungo cha mwaka mmoja jela," kimeeleza kifungu hiko.

Aidha kifungu hiko kinatanabaisha kuwa adhabu hiyo atapatiwa mtu ambaye atafanya hayo kwa makusudi bila kuwa na idhini ya mamlaka.

Hata hivyo sheria hiyo haihusishi fedha zinazoharibika kutokana na matumizi ya muda mrefu au mazingira mengine yasiyo ya makusudi huku fedha zilizoharibika zinaweza kuwa na sababu mbalimbali na, pale zinapotimiza masharti, zinaweza kupokelewa na kubadilishwa.

Hapa ndipo tofauti ya kisheria na kiutendaji inapokuwa muhimu. Uharibifu wa kawaida unaotokana na matumizi si sawa na kuchukua noti na kuikata kwa makusudi, kuichora au kuiharibu kwa nia ya kuiondoa kwenye hali yake ya kawaida.

BoT imeendelea kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuheshimu fedha ya Tanzania ambapo kupitia elimu mbalimbali inazozitoa kwa umma na makundi ya wadau wake Benki Kuu inasisitiza kuwa vitendo vya kuharibu au kuidhihaki noti na sarafu ni kosa la jinai.

Kwa nini sheria imeweka ulinzi huo?

Kwanza, noti si karatasi ya kawaida. Benki Kuu ya Tanzania ndiyo yenye mamlaka ya pekee ya kutoa noti na sarafu kwa matumizi nchini, na fedha hizo ndizo zinazotumika kama fedha halali ya malipo.

Pili, fedha ina mfumo wa usimamizi unaohitaji uendelee kwa ufanisi kutoka hatua moja hadi nyingine. Benki Kuu husimamia utoaji wa noti, usambazaji wake kupitia mfumo wa benki na ukusanyaji wa fedha zilizotumika ili kutenganisha zile zinazofaa kuendelea kuwa katika mzunguko na zile ambazo zimekuwa chakavu.

Katika mazingira hayo, kitendo cha mtu kuharibu noti kwa makusudi kinaongeza mzigo kwenye mzunguko wa fedha. Noti hiyo inaweza kuhitaji kuondolewa, kuchakatwa na kubadilishwa na nyingine inayoweza kutumika.

Sheria pia inaweka utaratibu kuhusu fedha zilizopotea au kuharibika ambapo kifungu cha 29 (1) (2) (3) (4) cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwaka 2006;

"Hakuna mtu atakayekuwa na haki ya kudai kutoka Benki thamani ya noti au sarafu yoyote iliyopotea, kuibiwa au isiyokamilika, au noti yoyote iliyoharibiwa, au sarafu yoyote ambayo imechezewa au kubadilishwa kwa namna isiyoruhusiwa."

"Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kuamua thamani yoyote ambayo inaweza kulipwa kwa mtu anayewasilisha Benki noti ambayo imekumbwa na mojawapo ya hali zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1)."

"Mazingira ambayo, pamoja na masharti na mipaka ambayo thamani ya noti au sarafu iliyopotea, iliyoibiwa au isiyokamilika, au noti iliyoharibiwa, au sarafu ambayo imechezewa, inaweza kurejeshwa kwa hiari ya Benki, yataamuliwa kwa uamuzi wa pekee wa Benki."

"Kwa madhumuni ya kifungu hiki, sarafu itachukuliwa kuwa imechezewa au kufanyiwa mabadiliko yasiyoruhusiwa iwapo imeharibika, imepunguzwa au kupunguzwa uzito kwa namna ambayo si matokeo ya uchakavu wa kawaida wa matumizi. Pia, sarafu itachukuliwa kuwa imechezewa iwapo imeharibika kwa kuchapwa alama, kuchongwa maandishi au kutobolewa, bila kujali kama hatua hiyo imesababisha kupungua kwa ukubwa au uzito wake,"kimeeleza kifungu hiko.

Mbali na kifungu cha 332A cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, sheria za Tanzania zina masharti mengine kuhusu uhalali na usalama wa fedha. Hii ni pamoja na makosa yanayohusisha kughushi au kutengeneza vifaa kwa ajili ya kughushi fedha, ambayo yana adhabu tofauti na kubwa zaidi.



BOT INAVYOCHAGIZA ELIMU YA UTUNZAJI WA NOTI KWA WANANCHI

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeendelea kuimarisha elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza noti katika hali salama, ikisisitiza kuwa utunzaji mzuri ni sehemu muhimu ya kulinda ubora wa noti.

Benki hiyo inasema elimu kuhusu fedha hutolewa kupitia programu mbalimbali za kufikia makundi mbalimbali na jamii kwa ujumla.

Akizungumza na jarida hili, Meneja Msaidizi wa Uhusiano kwa Umma BoT, Bi. Noves Moses anasema miongoni mwa njia zinazotumika kufikisha elimu hiyo kwa jamii ni pamoja na maonesho mbalimbali, semina za makundi maalumu, mikutano ya hadhara, vipindi vya redio na runinga na maudhui mbalimbali kupitia mitandao ya kijamii.

"Katika njia hizo za kufikisha elimu kuhusu utunzaji sahihi wa noti, wananchi hupata fursa ya kuuliza maswali kuhusu fedha, kazi za Benki Kuu na namna ya kuitumia fedha kwa usalama. Kwa upande wa noti, elimu inalenga mambo mawili yanayohusiana kwa karibu, ambayo ni kuhifadhi fedha vizuri na kuweza kutambua noti halali,"anasema Bi. Noves

Elimu hiyo inaenda sambamba na haki za mteja ambapo BoT kupitia nyaraka ya haki na wajibu wa mteja imeeleza namna ambavyo mteja ana wajibika kutunza fedha hizo.

"Mwananchi ana haki ya kupewa noti safi kutoka kwa karani wa benki au mashine za kutolea fedha, na pia anaweza kuweka benki noti safi au zilizochafuliwa,"imeeleza nyaraka hiyo.

Hata hivyo, elimu ya utunzaji wa noti haijatenganishwa na elimu ya kupambana na fedha bandia. BoT imekuwa ikitoa mafunzo kwa wadau wa sekta ya fedha kuhusu alama za usalama zilizopo kwenye noti ili kuwajengea uwezo wa kutambua fedha halali na kuzuia matumizi ya noti bandia.

Bi. Noves amesema elimu hiyo imekuwa pia ikiwafikia makundi mbalimbali kila robo mwaka.

"BoT haijawa nyuma katika eneo hili, kwa mfano robo mwaka ya kwanza ya mwaka wa fedha 2026/2027, tumetoa elimu ya utuzanji sahihi kwa kundi la wasanii kupitia Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) na Bodi ya Filamu,"anasema Bi. Noves.

Hatua ya mafunzo hayo imetokana na mwenendo usioridhisha wa wasanii wa kutupa fedha chini wakati wa kutunzana katika sherehe mbalimbali wanazoziandaa.

Aidha, licha ya elimu kwa makundi mbalimbali, pia BoT imezielekeza benki za biashara kuwapa wateja taarifa kuhusu haki na wajibu wao katika miamala ya fedha taslimu. Kwa mtazamo huo, benki inakuwa sehemu ya kwanza ya kumsaidia mwananchi kuelewa namna ya kuhifadhi fedha na namna ya kushughulikia noti zilizoharibika.

Pia, BoT imekuwa ikitumia mafunzo kwa wadau kama njia ya kuzalisha waelimishaji wengi zaidi wa elimu ya fedha kupitia programu ya Watoa Elimu ya Fedha wa Jamii (CFE).

Katika upande wa Benki Kuu, elimu hiyo inaendelea kuwa sehemu ya usimamizi wa sarafu.

Kupitia tovuti yake, BoT inaeleza kuwa moja ya majukumu yake ni kuhakikisha kuna upatikanaji wa noti na sarafu zenye ubora unaokubalika na kwamba fedha zinaendelea kutumika kwa ufanisi katika shughuli za kiuchumi.

Akizungumzia ukomo wa elimu hiyo, Bi Noves anasema; "Elimu ya utunzaji wa noti si kampeni ya muda mfupi. Ni mchakato unaohusisha taasisi, sekta ya fedha na wananchi. Kadiri uelewa unavyoongezeka, ndivyo uwezekano wa fedha kutunzwa vizuri, kutambuliwa kwa usahihi na kubaki katika mzunguko kwa muda mrefu unavyoongezeka."

Licha ya kuendelea kutoa elimu hiyo ya utunzaji wa fedha, Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba katika mahojiano yake na jarida hili alisema kuwa njia mbadala ya kukabiliana na uchakavu wa noti ni kutumia mifumo ya malipo inayosimamiwa na BoT.

"Kwa sasa hivi dunia inaenda kidijitali, tunashauri wananchi wafanye malipo ya bidhaa zao kwa njia ya kidijitali, ambapo kupitia LIPA NAMBA, anaweza kununua bidhaa. Hiyo inasaidia kutozishika fedha taslimu mara kwa mara na kupunguza uchakavu,"alisema Gavana Tutuba.



Meneja Msaidizi wa Idara ya Mawasiliano BoT, Bi. Noves Moses, akizungumza katika moja ya vikao vya kujadili utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya utunzaji sahihi wa Noti za Tanzania.

KIBONZO

01



02



03



04



05



06



BOT YANG'ARA MAONESHO YA NANENANE

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeendelea kung'ara katika Maonesho ya Kilimo ya Nane Nane 2026 kwa kutoa elimu kuhusu masuala ya fedha na uchumi, huku ikitajwa pia kuwa miongoni mwa taasisi zilizofanya vizuri kwa kutwaa tuzo katika kanda mbalimbali nchini.

Maonesho hayo kitaifa yalifanyika jijini Dodoma ambapo, Naibu Gavana wa BoT anayeshughulikia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, alitembelea banda la Benki Kuu katika maonesho hayo jijini Dodoma Agosti 6, 2026 na kujionea shughuli za utoaji elimu na huduma kwa wananchi.

Katika ziara hiyo, Dkt. Mahfoudh alipatiwa maelezo kuhusu elimu inayotolewa kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa sera ya fedha, uwekezaji katika dhamana za Serikali, mifumo ya malipo ya taifa, usimamizi wa sekta ya fedha na utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za kifedha.

Pia alielezwa kuhusu fursa za ajira zinazotolewa na Benki Kuu pamoja na mafunzo yanayotolewa na Chuo cha Benki Kuu.

Dkt. Mahfoudh pia alielezwa kuhusu elimu inayotolewa kuhusu alama za usalama za noti za Tanzania na namna sahihi ya kutunza noti na sarafu ili kudumisha ubora na usalama wa fedha taslimu.

Akizungumza na wataalamu wa BoT katika banda hilo, Dkt. Mahfoudh aliwapongeza kwa juhudi wanazozifanya katika kuwahudumia wananchi na kusisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa weledi, uwazi na kutumia lugha rahisi inayoeleweka na makundi yote ya jamii.

Alisema elimu hiyo ni muhimu katika kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu majukumu ya Benki Kuu na kuwasaidia kutumia huduma za kifedha kwa usahihi.

"Elimu ya fedha ni nguzo muhimu katika kujenga jamii yenye uelewa wa masuala ya kifedha, hivyo kuwawezesha wananchi kufanya maamuzi yenye tija na kuchangia maendeleo endelevu ya uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla," alisema.

Maonesho ya NaneNane 2026 yaliongozwa na kaulimbiu "***Tambua Soko; Ongeza Tija Kutekeleza Dira 2050.***"

Matawi ya BoT yashiriki

Mbali na Dodoma, BoT ilishiriki pia Maonesho ya Nane Nane 2026 kupitia Makao Makuu ndogo Zanzibar, yaliyofanyika kuanzia Agosti 1 hadi 16, 2026 katika viwanja vya Dole na Kizimbani.

Kupitia ushiriki huo, Benki Kuu ilitoa elimu kwa wananchi kuhusu majukumu yake katika kusimamia utulivu wa uchumi na sekta ya fedha pamoja na mchango wake katika kukuza maendeleo endelevu ya Taifa.

Katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Tawi la BoT Mbeya lilitwaa ushindi wa kwanza katika Kundi la Mamlaka za Udhibiti.



Naibu Gavana, Dkt. Rahma Mahfoudh, pamoja na washiriki wa BoT katika Maonesho ya Nane Nane jijini Dodoma. Kushoto kwake ni Meneja Idara ya Sera za Kibajeti na Usimamizi wa Deni, Bw. Mgonya Benedicto na Meneja Mawasiliano BoT, Bi. Victoria Msina.

Tuzo hiyo ilikabidhiwa na Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, na kupokelewa na Mkurugenzi wa Tawi la BoT Mbeya, Dkt. James Machemba.

Kwa upande wa Kanda ya Kusini, Tawi la BoT Mtwara lilitwaa pia ushindi wa kwanza katika kundi hilo. Tuzo hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ayoub Mohammed Mahmoud, na kupokelewa na Mkurugenzi wa Tawi la BoT Mtwara, Moto Lubogi.

Kanda ya Kaskazini nayo haikuwa nyuma, baada ya Tawi la BoT Arusha kutwaa ushindi wa kwanza katika Kundi la Mamlaka za Udhibiti.

Tuzo hiyo ilikabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, CPA Amos Makalla, na kupokelewa na Mkurugenzi wa Tawi la BoT Arusha, Dkt. Charles Masenya.

Aidha, katika Kanda ya Ziwa, Tawi la BoT Mwanza lilipewa tuzo maalum ya udhamini katika maonesho hayo. Tuzo hiyo ilitolewa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mohamed Mtanda, na kupokelewa kwa niaba ya tawi na Meneja wa Idara ya Uendeshaji, Johnas Ezekiel.

Mafanikio hayo yamekuja wakati Benki Kuu ikiendelea kutumia maonesho na majukwaa ya umma kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi, kuwaongezea uelewa kuhusu masuala ya uchumi na fedha na kueleza nafasi ya taasisi hiyo katika kujenga mfumo imara wa fedha na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi wa Tanzania.

Kwa ujumla, ushiriki wa BoT katika maonesho hayo umeweka mkazo katika kuifikisha elimu ya fedha kwa wananchi kwa njia rahisi na shirikishi, huku matawi yake yakichangia kwa vitendo katika kufikisha ujumbe huo katika maeneo mbalimbali ya nchi.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. CPA Amos Makalla, akimkabidhi Mkurugenzi wa Tawi la BoT Arusha, Dkt. Charles Masenya, tuzo ya ushindi wa kwanza katika Kundi la Mamlaka za Udhibiti



Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar, akimkabidhi Mkurugenzi wa Tawi la BoT Mbeya, Dkt. James Machemba, tuzo baada ya BoT kupata ushindi wa kwanza katika kundi la Mamlaka za Udhibiti.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mohamed Mtanda, akimkabidhi Meneja wa Idara ya Uendeshaji, Bw. Johnas Ezekiel tuzo maalum ya udhamini katika Maonesho ya Nane Nane, yaliyofanyika katika viwanja vya Nane Nane, Nyamhongolo, jijini Mwanza.

GAVANA TUTUBA AKUTANA NA MWAKILISHI MPYA WA IMF NCHINI TANZANIA





Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amekutana na kufanya mazungumzo na Mwakilishi Mkazi Mpya wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nchini Tanzania, Bi. Jana Bricco, katika Makao Makuu ya Benki Kuu jijini Dodoma, Agosti 26, 2026.

Katika kikao hicho, Gavana Tutuba alieleza hatua mbalimbali zinazoendelea kutekelezwa na Benki Kuu katika kusimamia ukuaji na ustahimilivu wa uchumi, ikiwemo kuimarisha uthabiti wa thamani ya Shilingi, kuongeza akiba ya fedha za kigeni kupitia programu ya ununuzi wa dhahabu, pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha.

Kwa upande wake, Bi. Bricco aliipongeza Tanzania kwa kukamilisha programu mbili za kifedha za IMF, ambazo ni Extended Credit Facility (ECF), inayolenga kusaidia nchi kuimarisha uchumi kupitia upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu, na Resilience and Sustainability Facility (RSF), inayosaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha ustahimilivu wa uchumi. Programu hizo zimeiwezesha Tanzania kupata jumla ya Dola za Marekani milioni 443.9.

Akihitimisha kikao hicho, Gavana Tutuba aliahidi kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Benki Kuu na IMF, hususan katika kuendeleza sera na hatua zinazolenga kudumisha uthabiti wa uchumi na kukuza maendeleo endelevu nchini.

Gavana Emmanuel Tutuba, akielezea jambo katika kikao na Mwakilishi Mkazi Mpya wa IMF nchini Tanzania, Bi. Jana Bricco, kilichofanyika katika Makao Makuu ya Benki Kuu jijini Dodoma, tarehe 26 Agosti 2026.

WAZIRI MKUU AIPONGEZA BoT KWA UNUNUZI WA DHAHABU, USIMAMIZI WA UCHUMI

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, ameipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa namna inavyosimamia uchumi wa nchi, akitaja utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa dhahabu kuwa miongoni mwa hatua zinazochangia kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania.

Waziri Mkuu aliyasema hayo Oktoba 3, 2026, alipotembelea banda la BoT katika Maonesho ya Teknolojia ya Madini wakati wa shughuli za kuhitimisha maonesho hayo mkoani Geita.

"Mmetekeleza vyema mpango wa ununuzi wa dhahabu ambao umeifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye akiba ya dhahabu na ambayo imeanza kufanya kazi ya kuimarisha sarafu ya nchi,"alisema

Dkt. Mwigulu amesema uimara wa uchumi wa Tanzania umeonekana katika vipindi mbalimbali ambavyo dunia imekuwa ikikabiliwa na misukosuko ya kiuchumi, akieleza kuwa nchi imeendelea kuwa na uwezo wa kustahimili changamoto hizo.

"Katika rekodi za taasisi zote zinazofanya uchambuzi wa masuala ya kiuchumi, Tanzania imeendelea kuonekana kuwa na ustahimilivu wa kiuchumi katika vipindi vyote ambavyo dunia imeshuhudia mitikisiko ya kiuchumi;"alisema.

Awali, akimkaribisha Waziri Mkuu katika banda la BoT, Gavana Emmanuel Tutuba alisema Benki Kuu imetimiza miaka miwili tangu ilipoanza kutekeleza mpango wa ununuzi wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji nchini.

Kwa mujibu wa Gavana, katika kipindi hicho BoT imenunua jumla ya tani 35.4 za dhahabu, huku tani tano zikiwa tayari zimeuzwa.

Alisema mpango huo umekuwa na mchango katika kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania na kusaidia kuweka mazingira mazuri katika soko la fedha za kigeni.

Gavana alisema kuwa BoT imeendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wa madini kuhusu umuhimu wa kufanya uwekezaji katika shughuli nyingine za kiuchumi, kwa kuzingatia kwamba rasilimali za madini ni rasilimali zisizorejelezwa.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, akieleza jambo katika banda la Benki Kuu mbele ya Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba katika maonesho ya Teknolojia ya Madini.

GAVANA ATOA WITO KWA TAASISI ZA FEDHA

Kwa upande mwingine, akitembelea mabanda ya taasisi za fedha katika maonesho hayo Gavana Tutuba, alizitaka benki na taasisi za fedha nchini kuandaa bidhaa na huduma zinazolenga wachimbaji na wadau wengine wa sekta ya madini, akisema hatua hiyo itasaidia kuchochea ukuaji wa sekta hiyo na uchumi kwa ujumla.

"Hata hivyo, nitoe rai kwa wale ambao bado hawajaanzisha bidhaa kwa ajili ya wachimbaji kufanya hivyo, kwa sababu sekta hii ni fursa na ina mchango mkubwa katika uchumi wetu," amesema.

Gavana Tutuba alisema taasisi za fedha hazipaswi kuiona sekta ya madini kwa mtazamo wa vihatarishi pekee, bali zinapaswa kutafuta namna ya kuzirasimisha na kuzitumia fursa zilizopo ili kuongeza tija katika shughuli za uchimbaji.

Gavana Tutuba alitembelea mabanda mbalimbali ikiwamo; Banda la BoT, benki mbalimbali, Bodi ya Bima ya Amana, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA).

Maonesho hayo ya tisa ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini, yaliyofanyika kuanzia tarehe 23 Septemba hadi 03 Oktoba 2026 yamengozwa na kaulimbiu "Madini ni tajiri, tuwajibike kwa pamoja kufikia Dira ya Taifa 2050.



MAKAMU WA RAIS AAGIZA WIZARA TATU KUWAJENGEA UZOEFU VIJANA



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Deogratius Ndejembi ametoa wiki mbili kwa wizara tatu kuja na mpango wa kuchukua vijana takribani 10,000 na kuwajengea uzoefu katika ofisi zao.

Wizara zilizopewa maagizo hayo ni pamoja na; Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo ambapo wametakiwa kuandaa mpango wa mafunzo kwa vitendo ambao utaanza kuchukua walau vijana 10,000 kupata uzoefu ili kuwandaa na kujiajiri.

Makamu wa Rais ametoa maelekezo hayo wakati alipomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan, kwenye ufunguzi wa Kikao Kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma, kinachofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC).

Amewataka Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kubadili namna taasisi hizo zinavyofanya kazi na kuwa injini ya mageuzi ya uchumi kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, huku akielekeza kuanzishwa kwa mkakati huo utakaowapatia angalau wahitimu 10,000 nafasi za mafunzo kwa vitendo na kuwapatia fedha za kujikimu katika mashirika ya umma na wengine wasiopungua 20,000 katika sekta binafsi.

"Kila mwaka kwa takribani vijana 62,570 wanahitimu elimu ya juu na hii ni takwimu ya mwaka Jana 2025 toka TCU, idadi hiyo haihusishi wale wanaomaliza VETA na Vyuo vya Kati. Ukiangalia TAESA takwimu zao zinaonesha vijana 3,200 pekee walikuwa wamepitia programu za mafunzo internship, idadi hii ni ndogo sana kwa kulinganishwa na wahitimu 62,570 kutoka vyuo mbalimbali nchini.

"Mlitazame hili kama uwekezaji wa kimkakati katika nguvu kazi ya Taifa kwa kubana matumizi ya kawaida, na hapa mtakuwa mmetekeza kwa Vitendo nguzo ya pili ya Dira 2050" alisema na kuongeza.

Mhe. Ndejembi, alisisitiza kuwa dhamana ya Watendaji, Wakuu wa Mashirika na Wenyeviti wa Bodi ni kubwa, na hivyo wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa ustadi na umakini mkubwa na kwa wakati sahihi katika kujenga uchumi, kuibua fursa mpya na kuinua maisha ya watanzania.

ZANZIBAR YAITAKA URUSI KUSHIRIKIANA KATIKA SEKTA ZA KIMKAKATI



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar iko tayari kuimarisha ushirikiano na Shirikisho la Urusi katika sekta mbalimbali za kimkakati, ikiwemo nishati, uchumi wa buluu, bandari na usafirishaji, utalii, elimu, afya na utafiti.

Dkt. Mwinyi amesema hayo Septemba 28, 2026, alipokutana na ujumbe kutoka Shirikisho la Urusi ulioongozwa na Mkuu wa Kurugenzi ya Wataalamu katika Ofisi ya Rais wa Shirikisho la Urusi, Bw. Denis Agafonov, pamoja na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bw. James Kinyasi Millya.

Amesema Zanzibar inaona fursa kubwa ya kushirikiana na Urusi katika sekta ya nishati, hasa katika utafutaji na upatikanaji wa nishati, matumizi ya vyanzo mbadala pamoja na teknolojia ya nishati ya nyuklia.

Kwa mujibu wa Dkt. Mwinyi, tafiti za awali zimeonyesha uwepo wa rasilimali za mafuta na gesi asilia Zanzibar, hususan katika maeneo ya baharini, hivyo Serikali iko tayari kushirikiana na kampuni za Urusi zenye utaalamu na teknolojia katika shughuli za utafutaji, uchunguzi na uendelezaji wa rasilimali hizo.

Katika sekta ya bandari na usafirishaji, amesema nafasi ya kijiografia ya Zanzibar inatoa fursa ya kuimarisha biashara na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Amesema Serikali iko tayari kushirikiana na Urusi katika kuendeleza Bandari Jumuishi ya Mangapwani, ikiwemo kutumia utaalamu, teknolojia na uwekezaji wa Urusi ili kuongeza uwezo wa Zanzibar kuwa lango muhimu la biashara katika ukanda huo.



UVUVI, AFYA

Katika sekta ya uvuvi, Rais Mwinyi amesema Serikali iko tayari kushirikiana na Urusi katika kuimarisha sekta hiyo kupitia teknolojia, utaalamu na uwekezaji utakaosaidia kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao ya baharini.

Amesema katika sekta ya afya, Zanzibar inalenga kuongeza matumizi ya teknolojia za tiba kwa njia ya mtandao ili kuwaunganisha wagonjwa walioko katika vituo vya afya na wataalamu walioko katika vituo vya afya na hospitali za rufaa.

Akihitimisha, Dkt. Mwinyi ameshukuru ujumbe huo kwa kutembelea Zanzibar na kuonyesha dhamira ya kuendeleza ushirikiano kati ya Tanzania na Shirikisho la Urusi.

Amesisitiza umuhimu wa kugeuza maeneo yaliyobainika kuwa na fursa za ushirikiano kuwa miradi yenye matokeo yanayoonekana kwa wananchi.

Kwa upande wake, Bw. Agafonov amesema Urusi ina uzoefu na utaalamu mkubwa katika sekta mbalimbali, hususan nishati, na iko tayari kuendelea kujadiliana na Zanzibar kuhusu maeneo yenye fursa za ushirikiano na uwekezaji.

UTALII NAO WATAJWA

Akizungumzia utalii, Dkt. Mwinyi amesema Zanzibar inalenga kuongeza idadi ya watalii kutoka Urusi, hasa kwa kuimarika kwa safari za ndege za moja kwa moja kati ya Zanzibar na Moscow, sambamba na kuvutia uwekezaji zaidi katika miradi ya utalii.

Amesema Serikali iko tayari kushirikiana na wawekezaji kutoka Urusi katika miradi inayolenga kuongeza thamani ya sekta ya utalii, kukuza biashara na kupanua fursa za ajira kwa wananchi.

Kwa upande wa elimu, amesema Zanzibar inalenga kuimarisha ushirikiano wa muda mrefu na Urusi kwa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Tanzania, kuendeleza tafiti za pamoja na kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi stadi na utafiti.

Dkt. Mwinyi amesema ushirikiano huo unaweza pia kuhusisha sayansi na teknolojia ya bahari, hatua ambayo inaweza kusaidia kuongeza mkono utekelezaji wa sera na mipango ya Uchumi wa Buluu Zanzibar.



LIJUE SOKO LA FEDHA ZA KIGENI

Soko la fedha za kigeni ni mfumo unaomwezesha mteja kununua na kuuza sarafu za nchi mbalimbali, kwa upande wa Tanzania soko la fedha ni muhimu kwa kuwa Tanzania ni nchi inayojihusisha na biashara za kimataifa kama uwekezaji, utalii malipo ya bidhaa na miradi mikubwa.

Sarafu ya Tanzania, hubadilishwa dhidi ya sarafu nyingine kama vile Dola ya Marekani (USD), Euro (EUR) na Pauni ya Uingereza (GBP). Kiwango cha kubadilisha sarafu kinaathiriwa na mambo mbalimbali, kama mahitaji, upatikanaji wa fedha za kigeni, biashara ya kimataifa, utalii, uwekezaji na mwenendo wa uchumi.

Katika kukabiliana na athari za kutokuwepo kwa soko hilo, Benki Kuu ya Tanzania ambayo ina jukumu la kusimamia soko la fedha na kuhakikisha linafanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa, iliona umuhimu wa kuanzisha soko la fedha za kigeni baina ya Mabenki, Interbank Foreign Exchange Markert (IFEM).

Soko la Fedha za Kigeni limesaidia kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya fedha, kwa kuwa mabenki ya biashara yaliyohidhinishwa yanaweza kununua na kuuza fedha za kigeni huku kiwango cha kubadilisha fedha kikiongezeka kulingana na mahitaji au upatikanaji wa fedha katika soko.

Hata hivyo umuhimu wa soko hilo umekuja wakati Benki Kuu ya Tanzania imejidhatiti katika kutekeleza sera ya fedha ikiwa na lengo la kudhibiti mfumuko wa bei kwa kuhakikisha bidhaa na huduma hazipandi kwa kasi ili kulinda thamani ya fedha, kukuza uchumi, yaani kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mikopo nafuu kwa ajili ya shughuli za uzalishaji, uwekezaji, utulivu wa kifedha na kulinda uimara wa mfumuko wa kibenki katika taasisi za kifedha nchini, na kuweka viwango vya riba, shughuli za soko la wazi, kuuza au kununua dhamana za serikali ili kupunguza au kuongeza ukwasi.

Kutokana na usimamizi huo thabiti wa Benki Kuu, biashara hiyo ya fedha za kigeni inafanyika kwa mafanikio makubwa hapa nchini na kufanya benki zenye faida za kigeni kuuza kwa benki zenye mahitaji wakati Benki Kuu ikikusanya taarifa muhimu kuhusu miamala inayofanywa katika soko na kutoa taarifa muhimu kuhusu kiwango cha kubadilisha shilingi dhidi ya fedha za kigeni na kukokotoa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni.

Benki Kuu katika kuhakikisha soko la fedha za kigeni linaleta tija kwa nchi Mwaka 2026 ilianzisha mfumo wa Electronic Matching System (EMS) katika IFEM ambao unaoanisha oda za kununua na kuuza fedha za kigeni kwa njia ya kielectroniki hatua inayolenga kuongeza uwazi, ufanisi na urahisi wa biashara hiyo.

Kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai hadi Septemba Mwaka huu IEFM iliendelea kufanyika kwa mafanikio makubwa huku kasi ya miamala ikiongezeka na kufikia takribani milioni USD 563.29 na kiwango cha wastani cha kubadilisha fedha za kigeni kilibaki Shilingi 2,650 hadi 2660

Hata hivyo, mabadiliko ya mahitaji na upatikanaji wa fedha za kigeni yanaweza kusababisha mabadiliko katika thamani ya Shilingi dhidi ya Sarafu nyingine. Kwa hiyo, usimamizi mzuri ni nyenzo ya kuimarisha utulivu wa mfumo wa fedha na kuwezesha shughuli za kiuchumi.

Soko la Fedha lina umuhimu mkubwa katika uchumi kwa kuwa linaunganisha Tanzania na uchumi wa dunia kwa kuwezesha ubadilishaji wa sarafu na kufanya malipo ya kimataifa yawezekane, kuongeza uwazi na ufanisi katika biashara ya fedha za kigeni, linawezesha fedha za kigeni kusambazwa kutoka taasisi zenye ziada kwenda taasisi zenye mahitaji. kugundua kiwango cha kubadilisha fedha kinachoakisi hali ya soko, kuimarisha biashara, uwekezaji na shughuli za kimataifa, kutekeleza sera ya uchumi wa fedha na kusimamia soko la fedha hizo.

Tanzania ni nchi yenye uchumi wenye nguvu kutokana na usimamizi imara wa sera ya fedha unaofanywa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Bw. Emmanuel Tutuba ambaye anasimamia sera hiyo kwa vitendo na kuakisi kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 inayotaka sekta ya huduma za fedha na masoko ya mitaji kuwa miongoni mwa sekta tisa za fedha za kimkakati zitakazochochea ukuaji wa uchumi na uhimilivu wa kifedha wa taifa.

Dira hiyo inalenga huduma za kifedha na uchumi shindani, kujenga mfumo imara wa kifedha na masoko ya mitaji yenye ubunifu, uwazi na ufanisi ili kuvutia mitaji ya ndani na nje na kupunguza utegemezi wa nje, uthabiti na uhimilivu wa kiuchumi, kusimamia sekta ya fedha ili kuleta utulivu wa jumla wa kiuchumi, jambo ambalo linajumuisha kudhibiti mfumuko wa bei na kuimarisha ukwasi na akiba ya fedha za kigeni na ujumuishaji na masoko ya fedha ambao huboresha upatikanaji wa rasilimali za kifedha kwa wananchi na wafanyabiashara ili kuchochea uzalishaji, biashara za kikanda na kimataifa.

SOKO LA MITAJI LAPAA, CMSA YAELEZA SABABU

Soko la mitaji nchini limeendelea kukua nchini, huku thamani ya uwekezaji ikiongezeka kwa asilimia 46.09 na kufikia TZS75.5 trilioni katika kipindi cha mwaka kilichoishia Juni 2026.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Soko la Mitaji kwa Robo Mwaka ulioishia Juni 2026 iliyotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), thamani hiyo imeongezeka kutoka TZS 51.68 trilioni zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2025.

"Ongezeko hilo limetokana na mazingira wezeshi ya kisera, udhibiti na uendeshaji wa soko yaliyosaidia kuibuka na kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa mbalimbali za masoko ya mitaji,"imeeleza sehemu ya ripoti hiyo.

Aidha, ripoti hiyo imetaja sababu nyingine ni juhudi za CMSA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji pia zimechangia ongezeko la ushiriki wa wawekezaji wa ndani.

Bidhaa hizo zinajumuisha dhamana za mapato yasiyobadilika, ikiwamo hatifungani za kawaida na zinazozingatia misingi ya Sharia, pamoja na vipande vya mifuko ya uwekezaji wa pamoja na Mifuko ya Uwekezaji Inayouzwa Sokoni 'Exchange Traded Funds (ETFs).

Mtaji wa soko wapanda

Ripoti inaonyesha kuwa mtaji wa jumla wa soko umeongezeka kwa asilimia 79.1 na kufikia Sh35.18 trilioni Juni 2026, kutoka Sh19.64 trilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2025.

Wakati huohuo, DSE All Share Index (ASI), unaotumika kufuatilia mwenendo wa bei za hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), ulipanda kwa asilimia 72 kutoka pointi 2,353.8 hadi pointi 4,048.8.

"Ukuaji huo unaonyesha kuongezeka kwa thamani ya soko la hisa katika kipindi husika,"imeandika ripoti hiyo.

Miamala ya hisa yaongezeka

Katika kipindi cha robo mwaka kinachoishia Juni 2026, shughuli za biashara katika soko la hisa zilipungua katika idadi ya hisa zilizouzwa na kuongezeka kwa idadi ya miamala.

Ripoti inaonyesha kuwa jumla ya hisa milioni 104.8 ziliuzwa, ikilinganishwa na milioni 256.9 katika robo mwaka iliyotangulia, sawa na kupungua kwa asilimia 59.2.

Hata hivyo, idadi ya miamala iliongezeka kwa kiwango kikubwa, kutoka 126,506 katika robo mwaka iliyoishia Juni 2025 hadi kufikia 528,031 katika robo mwaka ya Juni 2026, sawa na ongezeko la asilimia 317.4.

"Ongezeko hilo la miamala linaashiria kuimarika kwa ukwasi wa soko na ushiriki wa wawekezaji, pamoja na kuongezeka kwa shughuli za biashara katika hisa,"imeeleza ripoti hiyo.

ETF zakua kwa zaidi ya asilimia 1,600

Eneo lililoonyesha ukuaji mkubwa zaidi ni soko la Exchange Traded Funds (ETFs), ambapo mtaji wa soko ulifikia TZS 187.5 bilioni Juni 2026, kutoka TZS 10.54 bilioni zilizorekodiwa Desemba 2025, sawa na ongezeko la karibia mara 18.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ukuaji huo umechangiwa na kuongezeka kwa imani ya wawekezaji, uelewa kuhusu bidhaa hiyo na ongezeko la mahitaji ya wawekezaji wanaotafuta fursa za kuwekeza katika bidhaa zinazowapa nafasi ya kutawanya uwekezaji wao katika maeneo mbalimbali ya soko.



Hati fungani za Serikali zaendelea kuvutia

Biashara ya hatifungani za Serikali katika soko la upili nayo iliongezeka katika kipindi hicho kwa asilimia 2.5.

Ripoti inaonyesha kuwa thamani ya biashara ya hatifungani za Serikali ilifikia TZS 1.76 trilioni, kutoka TZS 1.71 trilioni katika robo mwaka kama hiyo ya mwaka 2025.

CMSA inasema ongezeko hilo lilichangiwa na kuimarika kwa ukwasi wa soko, kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji na kuendelea kuwepo kwa mahitaji ya dhamana za Serikali.

Kwa upande wa hati fungani za kampuni, thamani ya biashara iliongezeka hadi TZS 6.05 bilioni kutoka TZS 3.02 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2025, sawa na ukuaji wa asilimia 100.7.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ongezeko hilo linaonyesha kuendelea kukua kwa hamu ya wawekezaji katika dhamana zenye mapato yasiyobadilika, hali iliyosaidiwa pia na kuongezeka kwa bidhaa kupitia uorodheshaji wa hati fungani mpya za kampuni.

Mifuko ya uwekezaji yapaa

Ripoti hiyo imeeleza kuwa "Mifuko ya uwekezaji wa pamoja (Collective Investment Schemes – CIS) nayo imeendelea kufanya vizuri, huku thamani halisi ya mali inayosimamiwa (Net Asset Value – NAV) ikiongezeka kwa asilimia 74.9."

Ripoti hiyo ya CMSA inaeleza kuwa ukuaji huo umetokana na kuanzishwa kwa mifuko mipya yenye ubunifu, mwenendo mzuri wa mali ambazo fedha za mifuko hiyo zimewekezwa, kuongezeka kwa imani ya wawekezaji pamoja na kuboreshwa kwa ufanisi wa uendeshaji wa wasimamizi wa mifuko.

Kwa upande wa mgawanyo wa soko, mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS ilichangia asilimia 86.2 ya thamani halisi ya mali inayosimamiwa na mifuko ya uwekezaji wa pamoja huku ikifuatiwa na mifuko inayosimamiwa na iTrust Finance Limited ilichangia asilimia 8.0, huku sehemu iliyobaki ikichangiwa na mifuko inayosimamiwa na wasimamizi wengine.

JINSI WAWEKEZAJI WA NDANI, VIJANA WALIVYOIPAISHA DSE



Mkurugenzi Mtendaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Bw. Peter Nalitolela, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Kielelezo cha Faida Rejea ya Dhamana za Serikali uliofanyika tarehe 07 Agosti 2026 katika ofisi za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Dar es Salaam.

Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) limeweka historia baada ya thamani ya jumla ya kampuni zilizoorodheshwa sokoni kuvuka TZS 40 trilioni kwa mara ya kwanza tangu shughuli rasmi za biashara kuanza mwaka 1998.

Takwimu zinaonesha kuwa thamani hiyo imepaa ikichangiwa kwa kiwango kikubwa na wawekezaji wa ndani huku wengi wakiwa vijana wenye umri wa miaka kati ya 21 hadi 30.

Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa kati ya Septemba 7 hadi 11 ambapo thamani ya soko la kampuni zilizoorodheshwa DSE iliongezeka karibia mara mbili kutoka TZS 21.34 trilioni Septemba 2025 hadi TZS 40.61 trilioni kipindi kama hicho.

Hata hivyo, nyuma ya rekodi hiyo kuna ongezeko la ushiriki wa wawekezaji wa ndani, kuimarika kwa shughuli za biashara, matumizi ya simu katika uwekezaji pamoja na kuongezeka kwa thamani ya baadhi ya kampuni kubwa zilizoorodheshwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa DSE, Bw. Peter Nalitolela, alisema mwenendo huo unaonyesha kuongezeka kwa hamasa ya wawekezaji, shughuli za biashara, ukwasi wa soko na utendaji mzuri wa kampuni zilizoorodheshwa.

“Utendaji huu unaakisi mchanganyiko wa imani kubwa ya wawekezaji iliyochochea ongezeko la shughuli za uwekezaji, kuimarika kwa ukwasi wa soko, ushiriki wa taasisi na utendaji mzuri wa kampuni zilizoorodheshwa,” alisema Nalitolela.

Wawekezaji wa ndani wafurika
Kwa muda mrefu, masoko ya mitaji katika nchi zinazoendelea yamekuwa yakitegemea kwa kiasi kikubwa wawekezaji wa kigeni. Hata hivyo, mwenendo wa hivi karibuni DSE unaonyesha kuwa wawekezaji wa ndani wanaendelea kuwa nguvu muhimu katika shughuli za soko.

Katika wiki ya Septemba 7 hadi 11, wawekezaji wa kigeni walichangia asilimia 0.15 pekee ya manunuzi ya hisa, huku wakihusika na asilimia 10.34 ya mauzo.

Hali hiyo ilisababisha mtiririko wa fedha kutoka kwa wawekezaji wa kigeni unaokadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 2.36. Pamoja na hali hiyo, soko liliendelea kukua kutokana na ushiriki mkubwa wa wawekezaji wa ndani

Wawekezaji wa ndani walichangia asilimia 99.85 ya manunuzi yote na asilimia 89.66 ya mauzo katika wiki hiyo.

Kutokana na mwenendo huo, mtaji wa soko unaomilikiwa na wawekezaji wa ndani uliongezeka kwa asilimia 5.84 ndani ya wiki moja na kufikia TZS 28.28 trilioni, kutoka TZS 13.55 trilioni Septemba 2025.

Takwimu hizo zinaonyesha nafasi inayoongezeka ya mifuko ya hifadhi ya jamii, taasisi na wawekezaji binafsi wa Tanzania katika kuamua mwenendo wa biashara na bei za hisa.

Nalitolela alisema ongezeko hilo ni sehemu ya upanuzi mpana unaoendelea katika soko la mitaji. “Kimsingi, tunaona mtaji zaidi, shughuli nyingi zaidi za biashara na ongezeko la thamani ya kampuni likiingia katika soko,” alisema Bw. Nalitolela.

Benki, kampuni kubwa zaongoza
Ongezeko hilo la thamani limechangiwa pia na utendaji mzuri wa baadhi ya kampuni kubwa zilizoorodheshwa DSE.

Katika kipindi hicho, sekta ya benki, fedha na uwekezaji uliongezeka kwa asilimia 704, huku kampuni ya TCCL ikipanda kwa asilimia 10.28, NMB Bank (asilimia 8.42), TCC (asilimia 6.67) na CRDB Bank (asilimia 6.23).

Ongezeko la bei za hisa za kampuni hizo lilisaidia kusukuma thamani ya jumla ya soko kuvuka kiwango cha TZS 40 trilioni. Mwelekeo huo umejengwa pia na kuongezeka kwa shughuli za biashara katika miaka ya hivi karibuni.

Mwaka 2025, thamani ya biashara ya hisa iliongezeka kwa asilimia 190.3 hadi kufikia TZS 663.75 bilioni, huku idadi ya hisa zilizouzwa ikiongezeka kwa asilimia 109.6 hadi hisa milioni 477.8.

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, thamani ya biashara ya hisa ilifikia TZS 571.1 bilioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 320.86 kutoka TZS 135.7 bilioni katika robo iliyotangulia.

Mabadiliko ya biashara yachochea soko
Ukuaji huo umeenda sambamba na mabadiliko katika mfumo wa uuzaji na upangaji wa bei za hisa. Juni 2025, DSE ilianzisha Volume Weighted Average Price (VWAP) kama bei rasmi ya kufunga biashara, sambamba na mabadiliko katika viwango vya ukomo wa mabadiliko ya bei.

Mfumo huo hutumia bei na kiasi halisi cha hisa zilizouzwa katika kuamua bei ya kufunga biashara, hatua inayolenga kufanya bei ziakisi kwa karibu zaidi mwenendo wa shughuli za soko.

Kufikia mwishoni mwa Juni 2026, thamani ya biashara ya hisa ilikuwa imefikia TZS 1.068 trilioni, ikiwa tayari imezidi kwa asilimia 61.94 thamani yote ya biashara iliyorekodiwa mwaka mzima wa 2025.

Hisa Kiganjani yachochea wawekezaji
Teknolojia nayo imebadili namna ambavyo Watanzania wanavyoshiriki katika soko la hisa.

Kupitia mfumo wa Hisa Kiganjani, wawekezaji wanaweza kununua na kuuza hisa kwa kutumia majukwaa ya kidijitali, hivyo kupunguza baadhi ya vikwazo vilivyokuwepo katika uwekezaji wa hisa.

Mwaka 2025, akaunti mpya 123,547 za uwekezaji katika soko la hisa yaani Central Depository System (CDS) zilifunguliwa na kufikisha jumla ya akaunti 740,639.

Thamani ya biashara kupitia simu pia iliongezeka kwa asilimia 656 hadi kufikia TZS 106.7 bilioni, huku karibu akaunti 95,000 za simu zikiongezwa. Kufikia robo ya pili ya mwaka 2026, Hisa Kiganjani ilikuwa imewaunganisha wawekezaji 267,144.

BW. Nalitolela alisema mfumo huo umeisaidia DSE kuwafikia zaidi wawekezaji vijana. “Tuna hamasa kubwa hasa kutokana na vijana. Idadi kubwa ya akaunti za Hisa Kiganjani ni za watu wenye umri wa miaka 21 hadi 30, jambo linaloonyesha kuwa teknolojia inatusaidia kuwafikia kizazi kipya cha wawekezaji.”

Alisema lengo ni kufanya uwekezaji katika DSE kuwa rahisi na unaopatikana kwa urahisi kwa kila Mtanzania, bila kujali mahali alipo.

Fursa za uwekezaji zaongezeka
Mbali na hisa za kampuni, DSE imeendelea kupanua bidhaa zinazopatikana kwa wawekezaji.

Mwaka 2025, Vertex International Securities ilizindua Exchange-Traded Fund (ETF) ya kwanza nchini, iliyokusanya TZS 6.8 bilioni.

iTrust EAC Large Cap ETF iliorodheshwa Januari 2026 baada ya kupata mahitaji yaliyokuwa mara 5 zaidi ya kiasi kilichokuwa kimetolewa. Kufikia Septemba 2026, thamani ya jumla ya ETF ilikuwa imefikia TZS 231 bilioni.

Wakati huohuo, hati za Sukuk zilizo katika soko, zikiwamo Zanzibar, Al Barakah na Mapato Sukuk, ziliongezeka hadi TZS 320.73 bilioni kutoka TZS 175.64 bilioni mwaka mmoja uliopita.

Bidhaa hizo zinawapa wawekezaji chaguo zaidi badala ya kutegemea ununuzi wa hisa za kampuni moja moja.

TZS 40 trilioni zina maana gani?
Kuvuka kwa DSE kiwango cha TZS 40.61 trilioni hakumaanishi kuwa soko hilo lina TZS 40 trilioni taslimu. Kimsingi, mtaji wa soko (market capitalisation) ni thamani ya jumla ya kampuni zilizoorodheshwa sokoni inayokokotolewa kwa kuzingatia bei za hisa zao na idadi ya hisa zilizopo.

Kwa hiyo, ongezeko hilo linaonyesha zaidi thamani ya soko ya kampuni zilizoorodheshwa pamoja na mwenendo wa bei za hisa, kuliko kiasi cha fedha kilichopo katika DSE.

Umuhimu wa hatua hiyo unaonekana katika ukuaji wa soko na ongezeko la ushiriki wa wawekezaji wa ndani.

Soko la hisa lenye shughuli nyingi linaweza kusaidia kuunganisha akiba ya watu binafsi na taasisi na kampuni zinazohitaji mtaji kwa ajili ya upanuzi wa biashara na uwekezaji.

Katika utekelezaji wa mipango ya muda mrefu ya maendeleo ya Tanzania chini ya Dira 2050, soko la mitaji linaweza kuwa sehemu muhimu ya kuunganisha akiba ya ndani na uwekezaji wenye tija.

KAMISHNA TIRA ASISITIZA SEKTA KUAKISI DIRA YA TAIFA 2050



Wakati nchi ikiendelea na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imewataka wadau wa sekta hiyo kuoanisha shughuli zao na dira hiyo.

TIRA imesema kufanya hivyo ni kuchochea ukuaji wa sekta na kuhakikisha huduma za bima zinakuwa jumuishi na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi.

Hayo yalielezwa na Kamishna wa TIRA, Dkt. Bhaghayo Saqware Septemba 24 2026, visiwani Zanzibar, wakati akifungua rasmi Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya ya Washauri wa Bima nchini (TIBA), ambapo alikuwa Mgeni Rasmi.

Mkutano huo wa siku mbili ulilenga kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya Jumuiya hiyo na sekta ya bima kwa ujumla.

Akizungumza katika mkutano huo, Kamishna Dkt. Saqware aliitaka TIBA kuhakikisha shughuli zake zinaunga mkono malengo ya Dira ya Taifa 2050, huku akisisitiza umuhimu wa sekta ya bima kujenga taswira chanya kwa jamii kupitia ulipaji wa madai kwa wakati, utoaji wa huduma bora na kuwahudumia wateja kwa utu.

Aidha, amesema Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) itaendelea kushirikiana kwa karibu na TIBA katika kuimarisha Jumuiya hiyo na kuboresha miongozo na sera mbalimbali zinazolenga maendeleo ya sekta.

"Mwelekeo wa TIRA ni kuhakikisha sekta ya bima inakuwa endelevu, inakua mwaka hadi mwaka, inazingatia maadili na inajitenga na vitendo vya udanganyifu katika shughuli za bima,"alisema Dkt. Saqware

Kwa upande wake, Rais wa TIBA, Bi. Elinipa Elias, alisema Jumuiya hiyo itaendelea kujiimarisha na kushirikiana na wadau wa sekta ya bima ili kuboresha utoaji wa huduma na kuchangia maendeleo ya sekta nchini.

Mkutano huo umehudhuriwa pia na viongozi mbalimbali kutoka TIRA, akiwemo Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Khadija Said.

Wakati kamishna akisisitiza kuendana na Dira, hali ya utendaji wa soko la bima limeendelea kukua na kuimarika katika nyanja mbalimbali kwa mujibu wa Taarifa ya utendaji wa soko la bima kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2021 hadi 2024

"Idadi ya watoa huduma za bima imeongezeka kutoka 993 mwaka 2021 hadi kufikia 2,425 Juni 2025, sawa na ongezeko la jumla la asilimia 144.2. Ongezeko hilo ni sawa na wastani wa asilimia 22.1 kwa mwaka,"imeeleza taarifa hiyo iliyopo katika tovuti ya TIRA.

Taarifa hiyo inaongeza kuwa katika kipindi hicho, Mamlaka imeongeza aina mpya ya watoa huduma ikiwa ni pamoja na watoa huduma za afya (HSPs), warekebishaji na watengenezaji magari (ARMs) na Watoa Huduma Kidijitali. Vilevile, kampuni za bima mtawanyo nchini zimeongezeka kutoka kampuni moja mwaka 2021 hadi kampuni nne mwaka 2025.

Pia, taarifa hiyo imeonesha kuwa mchango wa sekta hiyo katika mapato ya Serikali umeongezeka kwa asilimia 33 mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022.

"Mchango wa Sekta ya bima kwenye mapato ya Serikali kupitia kodi mbalimbali ikiwemo Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya Kampuni (corporate tax) pekee umeongezeka kutoka shilingi bilioni 137.7 mwaka 2022 hadi kufikia shilingi bilioni 183.1 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 33,"imeeleza sehemu ya taarifa hiyo.

Hebu Tunza Pesa Zetu

Mtu anayejipenda, usafi ni jadi yake,
Kote kule anakwenda, utanashati ni wake,
Na hadhi yake hupanda, ule mwonekano wake,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Umevalia vizuri, mwanaume mwanamke,
Nguo zakaa vizuri, pochi i mahali pake,
Mfukoni una heri, pesa zi mahali pake,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Unafanya manunuzi, tumia na usichoke,
Kwa yoyote matumizi, katika pochi zitoke,
Zimenyoka ziko wazi, na wala zisikunjike,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Noti zetu za shilingi, ni vema ieleweke,
Kutunza iwe msingi, ili zisiharibike,
Zitumike muda mwingi, na gharama zipunguke,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Tukitunza zinadumu, zisichafukechafuke,
Hizo zinatuhudumu, matumizi zitumike,
Hadi ufike msimu, wa kubadilishwa kwake,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.



Njia nyingine kutunza, pesa pia zitumike,
Mitandao naiwaza, vema sana itumike,
Taslimu twapunguza, ya kwamba zisitumike,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Kwa mitandao ya simu, jitahidi itumike,
Mawakala wahudumu, kwenda huko tusichoke,
Huduma benki zidumu, kwa malipo zitumike,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Tunapozitunza pesa, kwamba sana zitumike,
Hilo jambo jema hasa, vema sana tulishike,
Tutapunguza kugusa, gharama zisitumike,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Vibaya tukizishika, hivyo hivyo zitumike,
Mara zitaharibika, na gharama zitumike,
Zingine tengenezeka, upungufu uzibike,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Kutunza pesa vizuri, elimu hiyo ishike,
Ni ya wazi siyo siri, kwa maswali usichoke,
Benki Kuu i vizuri, na wewe uelimike,
Hebu tunza pesa zetu, zidumu zisichakae.

Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)

Limetolewa na Idara ya Mawasiliano
Benki Kuu ya Tanzania

Anuani:
Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete, 40184
S.L.P. 2303 Dodoma, Tanzania

Barua pepe:
botcommunications@bot.go.tz
info@bot.go.tz

Tovuti:
www.bot.go.tz